JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# SHERIA YA MTOTO
[SURA YA 13]

## TAFSIRI YA KANUNI MWENENDO WA MAHAKAMA YA WATOTO ZA MWAKA 2014

Toleo hili la Kanuni Mwenendo wa Mahakama ya Watoto za mwaka 2014, Tangazo la Serikali Na. 270 la tarehe 25 Julai, Mwaka 2014, ni Tafsiri rasmi iliyosanifiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuchapishwa kwa mujibu wa kifungu cha 84 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Mbalimbali, Sura ya 1.

Dar es Salaam
28 Aprili, 2016

GEORGE M. MASAJU,
*Mwanasheria Mkuu Wa Serikali*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 170 la tarehe 13/05/2016

# KANUNI ZA MWENENDO WA MAHAKAMA YA WATOTO ZA MWAKA 2014

## MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kanuni* *Jina*

### SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi ya Kanuni.
3. Tafsiri.

### SEHEMU YA PILI
LENGO, UANZISHWAJI NA MAMLAKA YA MAHAKAMA ZA WATOTO

4. Madhumuni ya Kanuni.
5. Utambuzi.
6. Jengo la Mahakama ya mtoto.
7. Mazingira ya Mahakama.

### SEHEMU YA TATU
MASHARTI YA JUMLA YA MWENENDO NA USIMAMIZI WA MAHAKAMA YA WATOTO

8. Uendeshaji wa mashauri.
9. Lugha ya Mahakama.
10. Masharti ya wakalimani.
11. Kuendesha kesi kwa faragha.
12. Uamuzi kuhusu umri.
13. Utoaji wa taarifa kwa mtoto kuhusu utaratibu.
14. Msaada wa kisheria na misaada mingine inayofaa.
15. Uteuzi wa mlezi.
16. Mamlaka ya hakimu kuendesha kesi.
17. Mambo ya kuingizwa katika jalada la kesi ya jinai.
18. Mambo ya kuingizwa katika jalada la shauri la madai.
19. Kupata na uchambuzi wa kumbukumbu za Mahakama.

## SEHEMU YA NNE
### UFUNGUAJI WA SHTAKA LA JINAI DHIDI YA MTOTO

20. Mwenendo wa Mahakama.
21. Kutolewa kwa hati ya wito.
22. Kukamatwa kwa mtoto.
23. Hati ya ukamataji.
24. Hati ya mashitaka.
25. Mahudhurio ya wazazi, walezi au waangalizi.
26. Mzazi, mlezi au mwangalizi.
27. Shauri kutoendeshwa bila uwakilishi wa mtoto.
28. Dhamana.
29. Kuwekwa mahabusi.
30. Tathmini ya awali ya mtoto.
31. Mapitio ya amri ya kuwekwa mahabusi.

## SEHEMUYA TANO
### KESI YA JINAI INAI DHIDI YA MTOTO

32. Kujibu shitaka.
33. Pale ambapo mshtakiwa anakubali kosa.
34. Muda wa kuendeshwa kwa kesi ya jinai.
35. Ushiriki wa mtoto katika mwenendo.
36. Jukumu la kuweka wazi kesi ya upande wa mashtaka.
37. Usikilizwaji wa awali.
38. Kuahirishwa kwa shauri kutokana na kutohudhuria kwa wahusika au mashahidi.
39. Ushahidi wa upande wa mashtaka.
40. Kupokelewa kwa ushahidi wa kitabibu.
41. Kupokelewa kwa ushahidi wa maungamo.
42. Utetezi.
43. Ushahidi mkuu wa mtoto mshitakiwa.
44. Mamlaka ya Mahakama kuamuru utolewaji wa ushahidi.
45. Udadisi wa mashahidi.
46. Mtoto kutiwa hatiani.
47. Taarifa ya uchunguzi wa kijamii kabla ya hukumu.
48. Hukumu.

SEHEMU YA SITA

HUKUMU


49. Utaratibu wa kutoa hukumu.
50. Kuachiwa kwa masharti.
51. Faini, fidia na gharama.
52. Amri ya kuwekwa chiniya uangalizi.
53. Ukiukajia wa amri ya kifungo cha nje.
54. Amri ya kupelekwa katika shule ya maadilisho.


SEHEMU YA SABA

MALEZI


55. Maombi ya ulezi.
56. Utaratibu wa kufanya maombi ya ulezi.
57. Waombaji wa amri ya malezi.
58. Mamlaka ya kukataa maombi.
59. Wahusika katika mwenendo.
60. Tangazo na wito wa uombaji.
61. Vipimo vya Vinasaba na vipimo vya kitabibu.
62. Yaliyomo katika taarifa ya kipimo cha Vinasaba.


SEHEMU YA NANE

UANGALIZI NA KUMTEMBELEA MTOTO


63. Utaratibu wa kufanya maombi ya uangaalizi au kumtembelea mtoto.
64. Mamlaka ya Mahakama kuzingatia maombi ya uangalizi au kumtembelea mtoto
65. Uwasilishwaji wa maombi.
66. Maombi ya dharura ya kurejeshwa kwa mtoto.
67. Mambo ya kuzingatiwa wakati wa utoaji wa amri ya upande mmoja.
68. Amri ya muda inayotolewa kwa upande mmoja.
69. Kusikilizwa kwa mara ya kwanza.
70. Kuunganishwa kwa mtoto kwenye mwenendo.
71. Kuhamishwa.
72. Amri ya kutolewa kwa taarifa ya uchunguzi wa kijamii kuhusu uangalizi na kutembelea mtoto.
73. Mambo ya kuzingatia wakati wa utolewaji wa amri ya uangalizi na kumtembelea mtoto.
74. Mamlaka ya Mahakama kutoa amri kwa hiari yake.

75. Masharti kwa mtu aliyena amri ya uangalizi.
76. Amri za kutembelea mtoto.
77. Mambo ya kuzingatiwa wakati wa kutoa maombi ya kutembelea mtoto.
78. Kuondolewa kwa Amri zilizopo.
79. Kubadilisha amri ya uangalizi au amri ya kumtembelea mtoto.
80. Katazo la kufanyika kwa maombi mengine bila idhini maalum ya Mahakama.
81. Amri za utekelezaji.
82. Kuondolewa kwa mtoto kutoka katika Jamhuri ya Muungano.

## SEHEMU YA TISA
### MATUNZO

83. Maombi ya Amri ya matunzo.
84. Mambo ya kuzingatiwa wakati wa utoaji wa amri ya mwanzo.
85. Taarifa ya uchunguzi wa kijamii ya matunzo.
86. Malipo ya matunzo ya mtoto.
87. Utekelezaji wa matunzo ya mtoto.
88. Kubadilishwa na kuondolewa kwa amri ya matunzo.

## SEHEMU YA KUMI
### KINGA, MALEZI NA UTARATIBU WA USIMAMIZI WA MTOTO

89. Uvunjaji wa haki ya mtoto.
90. Mtoto anayehitaji ulinzi.
91. Maombi ya amri ya malezi na uangalizi.
92. Kusikilizwa kwa mara ya kwanza wa maombi.
93. Maombi ya kujumuishwa kama mjibu hoja.
94. Amri ya muda ya malezi au uangalizi.
95. Ushahidi wa kitaalam.
96. Wahusika kukubaliana kuhusu maelezo.
97. Wahusika kusikilizwa.
98. Amri zinazoweza kutolewa kufuatia maombi ya amri ya uangalizi.
99. Mtoto kuwa huru kuasiliwa.
100. Vigezo vya kutolewa kwa amri ya uangalizi.
101. Haki ya wazazi chini ya amri ya malezi.
102. Kuweka utaratibu wa kumtembelea mtoto aliyechini ya amri ya uangalizi.
103. Maombi ya amri ya kumtembelea mtoto aliyechini ya uangalizi.
104. Muda wa amri ya malezi.
105. Maombi ya amri ya kuendelea na uangalizi.

106. Kuondolewa kwa amri ya uangalizi.
107. Amri ya usimamizi.
108. Amri zinazoweza kutolewa katika maombi ya amri ya usimamizi.
109. Muda wa amri ya usimamizi.
110. Mamlaka ya usimamizi.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
AMRI YA UPEKUZI NA KUTOA

111. Maombi ya amri ya upekuzi na kutoa.
112. Mamlaka ya Mahakama baada ya kutolewa kwa maombi ya amri ya upekuzi na kutoa.
113. Amri ya upekuzi na amri ya kutoa inayotolewa kwa upande mmoja.
114. Utaratibu wa utolewaji wa amri ya upekuzi na kutoa kwa pande zote.
115. Kusimamishwa kwa maombi ya amri ya malezi na uangalizi.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
AMRI YA UTENGAJI

116. Maombi ya amri ya utengaji.
117. Maombi ya amri ya kuzuia inayotolewa kwa fadhila ya upendeleo.
118. Vigezo vya utoaji wa amri ya utengaji.
119. Masharti ya amri ya utengaji.
120. Muda wa amri ya utengaji.
121. Kugeuza au kufuta amri ya utengaji.
122. Ukiukwaji wa amri ya utengaji.

SEHEMU YA KUMI NA TATU
RUFAA

123. Rufaa.

SEHEMU YA KUMI NA NNE
MASHARTI YA JUMLA

124. Marekebisho na uandaaji wa majedwali.
125. Kufutwa kwa kanuni.

**MAJEDWALI**

SHERIA YA MTOTO
(SURA YA 13)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 99(1))*

KANUNI ZA MWENENDO WA MAHAKAMA YA WATOTO ZA MWAKA 2014

## SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1.** Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Mwenendo wa Mahakama ya Watoto, mwaka 2014.

Matumizi ya kanuni

**2**. Isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo, kanuni hizi zitatumika kwa kesi zote zilizoko Mahakamani.

Tafsiri

3. Katika kanuni hizi isipokuwa kama mukhtadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 13

" Sheria" ina maana, Sheria ya mtoto;

"makazi" maana yake ni makazi yanayotolewa kwa kipindi cha mfululizo cha zaidi ya saa ishirini na nne;

"mtoa huduma ya makazi" maana yake ni mlezi wa kambo au makao yaliyoidhinishwa kwa mujibu wa sheria ya mtoto;

"muombaji" maana yake ni mtu anayewasilisha maombi ya madai katika Mahakama ya mtoto;

"maombi" maana yake ni namna ambavyo shauri, ama la jinai au madai, yanavyofunguliwa katika Mahakama ya mtoto, na inajumuisha hati ya maombi, wito wa Mahakama, au malalamiko;

"mlezi" maana yake ni mtu yeyote mwenye jukumu la siku hadi siku la kumlea mtoto aidha wakati wa kuwasilisha maombi au wakati shauri linaendeshwa mtu aliyekuwa anajukumu la kumlea mtoto kabla ya shauri halijafunguliwa;

"maombi ya ulezi wa mtoto" maana yake ni maombi ya uangilizi, kumtembelea mtoto, malezi na maombi yanayofanyika chini ya kifungu cha 95 cha Sheria ya Mtoto;

"upendo kwa mtoto" maana yake ni mchakato wowote, mtazamo, mazingira na matendo ambayo ni ya kiutu, yenye huruma na yenye maslahi kwa mtoto;

"mwenendo wa madai" maana yake ni maombi kuhusu malezi na usalama wa mtoto, malezi, matunzo, uangalizi na kumtembelea mtoto, kutenga, na upekuzi wa kumtoa mtoto;

Sura ya 33 "Kanuni" maana yake ni sheria ya mwenendo wa madai;

"Mahakama" maana yake ni Mahakama ya mtoto iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 97 cha Sheria;

"mwenendo wa Mahakama" maana yake ni hatua zozote zinazochuliwa na Mahakama kuanzia mtoto anapofikishwa Mahakamani kwa mara ya kwanza kwa shtaka la jinai dhidi yake mpaka maamuzi ya mwisho ya Mahakama, au kuanzia shtaka la madai kuhusiana na mtoto linapofunguliwa mpaka hukumu ya mwisho inapotamkwa;

"kutengwa kwenye makazi" maana yake ni mtoto asiye na malezi kutokana na kufukuzwa nyumbani na wazazi wake au kutokana na matendo ya wazazi yanayomfanya mtoto asiwe na namna nyingine bali kuondoka;

"taasisi inayofaa" maana yake ni makazi yaliyothibitishwa kwa ajili ya watoto walioathirika kijamii na watoto wa mitaani au taasisi inayotoa malezi na uangalizi kwa mtoto na haihusiani na mahabusu ya mtoto au shule ya maadilisho;

"familia ya kambo" maana yake ni familia ambayo mtoto analelewa kwa mujibu wa Kanuni za malezi ya kambo;

"mlezi" maana yake ni mtu aliyechukua jukumu au aliyeteuliwa kuwakilisha na kulinda maslahi ya mtoto kwenye shauri lililo kwenye Mahakama ya mtoto;

"madhara" maana yake ni iliyoainishwa chini ya kanuni za kinga ya mtoto;

"kusikiilizwa" ina maana sehemu yoyote ya shauri lililo kwenye Mahakama ya mtoto;

"uchunguzi wa awali" maana yake ni uchunguzi chini ya Kanuni za Kinga ya Mtoto inayofanyika kutathmini iwapo mtoto anaathirika au yuko katika mazingira yanayopelekea kuathirika kuliko kithiri;

"mtu mwenye maslahi" maana yake ni ndugu au mtu anayetambulika kwa tafsiri ya neno mwakilishi;

"Serikali za Mitaa" maana yake ni iliyotumika chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (mamlaka za wilaya) au sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);

"Hakimu" maana yake ni Hakimu Mkazi;

"kosa" maana yake ni kosa lolote lililoainishwa kwenye Sheria ya Kanuni ya Adhabu au Sheria nyingine zozote;

"amri" maana yake ni hati ya kukamatwa, wito au mchakato mwingine wa aina hiyo, na maamuzi ya mapitio au amri ya kuthibitisha matamko yoyote mengine rasmi yanayotokana na maamuzi ya Mahakama;

"sehemu ya usalama" maana yake ni mtoto kulelewa na ndugu, mtu anayefaa, makazi ya kambo, makazi yaliyothibitishwa au sehemu yoyote nyingine ambayo mtoto anaweza kupata hifadhi salama wakati akisubilia maamuzi ya Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii au Mahakama kuhusiana na malezi ya kudumu, isipokuwa haihusishi sehemu yoyote ya kumweka kizuizini ikijumuisha rumande, Mahakama ya watoto, shule ya maadilisho au gerezani;

"mwenendo wa kesi" maana yake ni maombi merejeo, madai, usikilizwaji wa shauri, kesi, rufaa au mapitio aidha ya kudumu au ya mpito baina ya wadai;

"mwakilishi" maana yake ni mzazi, mlezi, wakili au mlezi wa kuteuliwa na Mahakama anayemsaidia au kumwakilisha mtoto wakati shauri likiendeshwa Mahakamani;

"madhara yaliyokithiri" maana yake ni iliyotumika chini ya Kanuni za Kinga ya Mtoto;

"taarifa ya uchunguzi wa kijamii" maana yake ni taarifa iliyoandaliwa na Idara ya Ustawi wa Jamii kwa maelekezo ya Mahakama ya mtoto;

"uchunguzi wa kijamii" maana yake ni uchunguzi unaofanywa na Idara ya Ustawi wa Jamii;

"ripoti ya uchunguzi wa kijamii" maana yake ni ripoti ya maandishi iliyoandaliwa baada ya uchunguzi wa kijamii kukamilika; na

"Idara ya Ustawi wa Jamii" maana yake ni sehemu, kitengo, idara au chombo kingine cha usimamizi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa chenye jukumu la kutoa kinga kwa mtoto.

## SEHEMU YA PILI
### LENGO, UANZISHWAJI NA MAMLAKA YA MAHAKAMAYA WATOTO

Madhumuni ya Kanuni

**4.**-(1) Lengo la Kanuni hizi ni kuanzisha mfumo wa Utendaji na mwenendo unaowiana wa Mahakama za Watoto za Tanzania Bara na kuhakikisha kuwa haki za mtoto chini ya sheria zinazolindwa.

(2) Mahakama, katika kutekeleza mamlaka yoyote yaliyotolewa kwake chini ya Kanuni hizi au katika kutafiti kanuni yoyote, itazingatia lengo la Mahakama ya Watoto.

Utambuzi

**5.** Kila Mahakama ya watoto chini ya Sheria hii itatambulika kwa jina lake mahsusi na mahali au eneo.

Jengo la Mahakama ya mtoto

**6.**-(1) Pale ambapo hakuna jengo mahsusi la Mahakama zaidi ya jengo la kawaida linalotumika kwa ajili ya usikilizwaji wa kesi kwa ajili au dhidi ya watu wazima, mahakama-

(a) itakaa katika chumba cha Mahakama kilichotengwa au katika chumba cha hakimu; au

(b) kwa kadri itakavyowezekana, itakaa katika muda tofauti na wa mahakama ya watu wazima ambao utapangwa utakaopangwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi.

(2) Mpangilio wa Mahakama na utaratibu wa usikilizwaji wa mashauri, kwa kadri itakavyowezekana itakuwa kwa mujibu wa kifungu cha 7.

(3) Pale ambapo Mahakama inakutana katika jengo hilohilo la Mahakama linaloendesha kosa dhidi ya watu wazima, Afisa Msajili atahakikisha watoto wanaohudhuria Mahakama hiyo hawatumii chombo hicho hicho cha kusubiria au eneo linaloshikilia watu wazima wanaotuhumiwa makosa ya jinai.

Mazingira ya Mahakama

**7.**-(1) Ili kubainisha utaratibu usio rasmi na rafiki unaowezesha ushiriki mkubwa wa mtoto, washiriki wote watakaa kwa usawa na mtoto hatawekwa kizimbani au katika sehemu iliyonyanyuka.

(2) Wakati mtoto anashtakiwa kwa kosa la jinai, Mahakama itapangwa kwa utaratibu ufuatao-

(a) hakimu ataketi kwenye meza kuu;

(b) karani ataketi karibu na hakimu;

(c) mwendesha mashtaka ataketi upande wa kuume wa hakimu**;**

(d) mtoto ataketi pembeni ya Wakili wake au mlezi aliyeteuliwa na Mahakama ili kuweza kuwasiliana naye, muda tofauti na wa Mahakama ya watu wazima utakaopangwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi.

(e) Wakili wa upande wa utetezi, au pale ambapo hakuna wakili, mlezi aliyeteuliwa na Mahakama ataketi kushoto mwa hakimu;

(f) mtoto ataketi pembeni mwa wakili wake au mlezi aliyeteuliwa na Mahakama ili kuweza kuwasiliana naye;

(g) iwapo mtoto hana wakili au mlezi alieyeteuliwa na Mahakama, lakini mzazi au mlezi wake yupo, mzazi wake ataketi kushoto kwa hakimu;

(h) iwapo mtoto ana Wakili au mlezi alieyteuliwa na Mahakama, mzazi ataketi upande wa pili wa mtoto;

(i) afisa ustawi wa jamii atakaa mwishoni mwa meza mkabla na hakimu, isipokuwa kwamba, iwapo mtoto hana mzazi, afisa ustawi wa jamii ataketi katika nafasi ya mzazi;

(j) mtoto ataruhusiwa kuketi muda wote wa mwenendo wa kesi; na

(k) mtoto ataruhusiwa kuwasiliana na wakili wake au mlezi aliyeteuliwa na Mahakama wakati wowote wa mwenendo wa kesi.

(3) Mahakama inaweza kumtaka shahidi kutoa ushahidi akiwa kwenye kizimba cha shahidi.

(4) Pale ambapo muathirika wa kosa ni mtoto, Mahakama inaweza kubadili mazingira ya Mahakama na kuruhusu mpangilio wa kukaa ambao ni tofauti na ulioainishwa katika Kanuni ndogo ya (2) ili kuwezesha utoaji wa ushahidi wa mtoto ambaye ni shahidi.

(5) Maafisa wa Mahakama ya watoto kama mahakimu, mwendesha mashtaka, mawakili na maafisa wengine watavaa majoho rasmi au sare.

## SEHEMU YA TATU
### KANUNI ZA JUMLA ZA UTARATIBU NA USIMAMIZI WA MAHAKAMA YA WATOTO

Uendeshaji mashauri

**8.** Utaratibu wa Mahakama utakuwa siyo rasmi, rafiki kwa mtoto na utakaofanywa kwa njia ya uchunguzi bila kumhusisha katika taratibu zenye ushindani pale ambapo hatua hii italinda haki ya kisheria ya mtoto na wahusika wengine katika shauri.

Lugha ya Mahakama

**9.-**(1) Lugha ya Mahakama itakuwa ni Kiingereza na Kiswahili.

(2) Mahakama inaweza, kuendesha kesi, kwa kutumia Kiingereza au Kiswahili kwa kadri hakimu atakavyoelekezwa, isipokuwa kwamba iwapo mtoto hawezi kusoma au kuongea lugha inayotumika na Mahakama, atapewa mkalimani kwa mujibu wa kanuni ya 10.

(3) Mtoto hatatia saini katika nyaraka yoyote iliyoandikwa katika lugha asiyoielewa, isipokuwa kama nyaraka hiyo imetafsiriwa kwake, na amepewa fursa ya kujadiliana na wakili wake au mwakilishi.

(4) Mwenendo wote wa Mahakama na maamuzi yatarekodiwa kwa kiingereza.

Masharti ya wakalimani

**10.-**(1) Pale ambapo mtoto yuko yeye binafsi mbele ya Mahakama na ushahidi ukatolewa katika lugha asiyoielewa, ushahidi huo utatafsiriwa kwake katika lugha anayoielewa, ikiwemo lugha ya watoto viziwi, watoto wasioweza kuzungumza, utindio au ulemavu mwingine unaodhoofisha uwezo wa mtoto kuuelewa ushahidi.

(2) Pale ambapo mtoto anawakilishwa na ushahidi ukatolewa katika lugha tofauti na lugha ya Mahakama, na isiyoeleweka kwa mwakilishi, lugha hiyo itatafsiriwa kwa wakili, mwakilishi au mlezi aliyeteuliwa na Mahakama katika lugha ya Mahakama.

(3) Mahakama, kwa kupitia maombi yaliyofanywa na mtoto au mwakilishi wake, itatoa nakala ya hukumu na tafsiri ya hukumu hiyo katika lugha anayotumia mtoto kama huyo anaweza kutoa ushahidi katika lugha yake na lugha hiyo itatafsiriwa katika lugha ya Mahakama.

(4) Mahakama, kwa kupitia maombi yaliyofanywa na

mtoto au mwakilishi wake, itatoa nakala ya hukumu na tafsiri ya hukumu katika lugha ya mtoto kama atahitaji bila kucheleweshwa na bila gharama yoyote.

(5) Mahakama, kwa kupitia maombi yaliyofanywa ya mtoto au mwakilishi wake, itatoa nakala ya hukumu na tafsiri ya hiyo hukumu hiyo katika lugha ya mtoto kama atahitaji bila kucheleweshwa na bila gharama yoyote.

(6) Mahakama, itaweka orodha ya wakalimani.

(7) Pale ambapo mtu aliyerejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) na (3) hana mkalimani, hakimu anayeendesha shauri atamuomba hakimu mfawidhi kukmuainisha mkalimani mwenye sifa inayofaa kumsaidia.

(8) Mahakama itamuondosha mkalimani iwapo-

(a) tafsiri anayotoa iko chini ya kiwango kinachokubalika;

(b) mhusika au mtoto, wakili wa mtoto, mlezi aliyeteuliwa na Mahakama au mwakilishi mwingine hajaridhika na kiwango cha tafsiri kinachotolewa na kinachohitajika na endapo ameomba aondoshwe.

(9) Pale ambapo mkalimani ameondoshwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (8), mkalimani mbadala atateuliwa na Mahakama.

(10) Mahakama itamtaarifu mtu yeyote anayetoa tafsiri katika Mahakama kwamba-

(a) analo jukumu la kutunza siri kwa mtu anayemsaidia; na

(b) mwenendo wa kesi ni siri na kwamba hakuna taarifa kuhusu mwenendo wa kesi itakayotolewa kwa mtu wa tatu bila ridhaa ya Mahakama.

Sura ya 34

(11) Mahakama itamtaka mkalimani kula kiapo kwa mujibu wa Sheria ya Viapo.

Kuendesha kesi kwa faragha

**11**.-(1) Uendeshaji wa kesi zote Mahakamani utafanyika katika vyumba vya Mahakimu au vyumba vya Mahakama vya faragha.

(2) Chumba cha siri cha Mahakama kitatumika pale inapobidi ili kutunza siri na mienendo ya kesi isionekane au kusikika na watu wasioruhusiwa kuhudhuria kwenye shauri.

(3) Watu wanaoruhusiwa kuhudhuria ni pamoja na-

(a) afisa wa Mahakama;

(b) mawakili;
(c) maafisa ustawi wa jamii;
(d) mlezi aliyeteuliwa na Mahakama, rafiki wa katibu wa mtoto au mwakilishi mwingine;
(e) wazazi, walezi au waangalizi;
(f) mtoto ambaye ni muhisika wa shauri la madai, lakini siyo mshirika katika kesi, kwa ruhusa ya hakimu anayeendesha kesi;
(g) ndugu au rafiki wa mtoto kwa ruhusa ya hakimu anayeendesha kesi;
(h) watu wanaopenda kuhudhuria kwa lengo la kujifunza au kufanya utafiti watakaoruhusiwa na hakimu anayeendesha kesi;
(i) mtu yeyote mwingine ambaye hakimu anaona inafaa kutokana na mazingira yanayomhusu mtoto au mazingira yanayohitajika ili ili haki itendeke.

(4) Hakimu anayeendesha kesi, kabla ya kumruhusu mtu yeyote aliyetajwa chini ya aya za (g) na (h) ya kanuni ndogo ya (3) kuhudhuria katika mwenendo wa kesi, atapata ridhaa ya mtoto.

(5) Taarifa yoyote inayoweza kupelekea kumtambua mtoto anayehusika au aliyehusika na shauri la kesi ya jinai au madai katika Mahakama ya watoto haitachapishwa katika mfumo wowote wa matamshi, maandishi, muono au usio bayana bila ridhaa ya hakimu anayesikiliza kesi.

Uamuzi kuhusu umri

**12**.-(1) Pale ambapo mtu anayefikishwa mbele ya Mahakama anadai kuwa ni mtoto, na madai hayo yakibishaniwa, Mahakama itaelekeza uchunguzi ufanyike kuhusu umri wa mtoto chini ya kifungu cha 113 cha Sheria.

(2) Mahakama inaweza, katika kufanya uchunguzi chini ya kanuni ndogo ya (1), kuzingatia-
(a) cheti cha kuzaliwa cha mtoto;
(b) ushahidi wa kitabibu kwa kadri itakavyohitajika kuthibitisha kuzaliwa aidha ni wa kimaandishi au vinginevyo;
(c) taarifa za shule ya msingi aliyohudhuria mtoto kuhusiana na tarehe ya kuzaliwa ya mtoto;
(d) cheti chochote cha mtoto cha kuhitimu shule ya msingi au cheti cha aina hiyo; na
(e) taarifa nyingine yoyote ya kuaminika au nyaraka.

(3) Cheti cha kuzaliwa, isipokuwa kama kitapingwa, kitachukuliwa kutoa uthibitisho kamili wa kusadikika wa umri wa mtoto.

(4) Pale ambapo nyaraka zilizorejewa chini ya kanuni ndogo ya (2) hazipatikani au hazibainishi umri wa mtoto, Mahakama inaweza kutilia maanani ushahidi ufuatao-

(a) chanjo yoyote au kumbukumbu za kitabibu;

(b) uchunguzi wa kitabibu wa mtoto unaothibitisha umri, isipokukwa kwamba kipimo cha X-ray ya fuvu hakitatumika kama njia ya kubaini umri bila ridhaa ya Mahakama na ridhaa hiyo itatolewa katika mazingira ya kipekee tu;

(c) taarifa ya uchunguzi wa kijamii inayoombwa na Mahakama ya watoto kusaidia kuthibitisha umri wa mtoto.

(5) Afisa ustawi wa jamii, anapoandaa taarifa ya uchunguzi ya kijamii atamhoji mtoto na watu wengine wenye taarifa zinzohitajika kuhusu mtoto.

(6) Mahakama kwa madhumuni kumtambua mtoto, inaweza kuagiza kipimo cha nasaba kifanyike.

(7) Pale ambapo taarifa kuhusu umri siyo haijathibitisha kikamilifu kuhusu umri na kuna sababu za kuamini kuwa mtu huyo anaweza kuwa mtoto, itachukuliwa kuwa mtu huyo ni mtoto wa chini ya umri wa miaka 18.

(8) Pale ambapo Mahakama itaamua katika shitaka la jinai au shauri la madai kwamba mtu ambaye umri wake unabishaniwa ni mtoto na kuendelea kutoa uamuzi katika mazingira hayo, maamuzi, amri au hukumu ya Mahakama haitabatilishwa au kufunguliwa upya kutokana na maamuzi ya baadae au uthibitisho kwamba umri wa mtu huyo haukutamkwa kwa usahihi mbele ya Mahakama.

Utoaji wa taarifa kwa mtoto kuhusu utaratibu

**13.-(**1) Pale ambapo mtoto ni mhusika wa, au anahusishwa katika shauri la madai na amehudhuria katika usikilizwaji wa kesi Mahakamani, Mahakama itamfafanulia mtoto katika lugha anayoielewa-

(a) kiini cha maombi kilichotolewa na mambo ambayo hakimu atayaamulia;

(b) wajibu wa hakimu;

(c) kwamba ana haki ya kusikilizwa, yeye mwenyewe au

kupitia kwa wakili, mlezi aliyeteuliwa na Mahakama au mwakilishi mwingine; na

(d) utaratibu utakaofuatwa.

(2) Mahakama itamueleza-

(a) mtoto ambaye anahusika na kesi au mlengwa katika shauri; na

(b) mtu aliyehudhuria Mahakamani,

kuhusu hukumu iliyotolewa na madhara yake kwa mtoto

Msaada wa Kisheria na misaada mingine inayofaa

**14**.-(1) Mtoto ambaye ni mhusika katika shtaka la jinai au shauri la madai atakuwa na haki ya kupata huduma ya kisheria na misaada mingine inayofaa.

(2) Pale ambapo mtoto ambaye ni mhusika katika shauri hana uwakilishi wa kisheria, mwakilishi wa kisheria, uwakilishi huo utatolewa kwa mtoto bila gharama yeyote kwa wakati utakaohitajika.

Uteuzi wa mlezi

**15**.-(1) Pale ambapo mtoto hana uwezo wa kugharamia uwakilishi wa kisheria na haiwezekani kutoa huduma ya kisheria bure ya kwa mtoto, na mzazi au mlezi hana uwezo wa kutoa uwakilishi unaofaa kwa mtoto, hakimu **anayeendesha** shauri atahakikisha kwamba mtoto anayeshtakiwa kwa kosa la jinai anapewa msaada unaofaa kwa kupatiwa mlezi anayeteuliwa na Mahakama.

(2) Mahakama itamweleza mtoto aliyerejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) kwamba anaweza kuchagua kuwakilishwa na mzazi au kuiomba anaweza kuchagua mlezi aliyeteuliwa na Mahakama au kuiomba Mahakama imteue mtu huyo.

(3) Pale ambapo mtoto ni mhusika katika shauri la madai au anahusika na shauri la kinga ya mtoto, atawakilishwa na mlezi aliyeteuliwa na Mahakama, na atakuwa na haki ya kuwakilishwa kisheria.

(4) Mahakama itamruhusu mtoto ambaye ni mwathirika au ambaye ni shahidi katika shtaka la jinai na anayetoa ushahidi mbele ya Mahakama kusaidiwa na mlezi anayeteuliwa na Mahakama.

(5) Mahakama, kwa maombi yaliyorejewa chini ya Kanuni ndogo (4), inamteua mlezi pale ambapo uteuzi huo ni kwa maslahi ya mtoto.

(6) Mahakama itamruhusu mlezi aliyeteuliwa na Mahakama kumsaidia mtoto katika mahojiano ya mashahidi

kuwasilisha ushahidi wa kimaandishi au ushahidi mwingine kwa niaba ya mtoto na kuielezea Mahakama kuhusiana na mtazamo, matarajio na maslahi ya mtoto.

(7) Pale ambapo mlezi wa kuteuliwa na Mahakama wanatofautiana na mtoto anaweza kuomba kuruhusiwa kuchagua mlezi mwingine au Mahakama imchagulie mlezi mpya.

(8) Mahakama inaweza, kwa hiari yake yenyewe au kufuatia maombi yaliyofanywa na afisa ustawi wa jamii, kumuondoa mlezi wa Mahakama anayetenda kinyume na maslahi ya mtoto, na itamtaka mtoto kuchagua mlezi mpya au kumteua mlezi mpya wa Mahakama.

(9) Hakimu mfawidhi, kwa kushauriana na mkuu wa idara ya ustawi wa jamii wa wilaya ambayo Mahakama ipo, atahakikisha kwamba, wilaya ina idadi ya kutosha ya walezi wa kuteuliwa na Mahakama wenye sifa na uwezo wa kumsaidia mtoto.

(10) Mahakama itaweka orodha ya walezi wa kuteuliwa na Mahakama waliopo katika Wilaya.

Mamlaka ya hakimu kuendesha kesi

**16.-**(1) Katika kesi za jinai na madai, hakimu atakuwa na mamlaka ya-

(a) kuongeza na kufupisha muda wa kutekeleza amri au maelekezo;

(b) kutoa amri ya utoaji wa nyaraka;

(c) kuahirisha au kusogeza mbele usikilizwaji wa kesi;

(d) kumtaka mshiriki, au mwakilishi wa kisheria, wa mshiriki au mwakilishi mwingine kuhudhuria Mahakamani;

(e) kuelekeza kwamba sehemu ya shauri iendeshwe peke yake;

(f) kuahirisha kusikiliza kwa shauri zima au sehemu ya shauri au hukumu kwa ujumla au mpaka tarehe itakayopangwa au tukio fulani litakapotokea;

(g) kuunganisha mashauri;

(h) kusikiliza maombi au mashtaka mawili au zaidi kwa wakati mmoja;

(i) kuamua kwa mpangilio upi maombi, mashtaka au hoja zitasikilizwa;

(j) kuelekeza usikilizwaji wa maombi, shtaka au hoja kwa tofauti;

(k) kuzuia hoja isizingatiwe;
(l) kuendesha au kutoa uamuzi kuhusu ombi au shtaka baada ya uamuzi wa awali wa hoja;
(m) kuhamasisha washiriki kutumia utaratibu mbadala wa usuluhishi wa migogoro kwa kadri itakavyoonekana inafaa na kuwezesha utumiaji wa utaratibu huo;
(n) kuhakikisha kwamba orodha ya kesi inatoa angalau taarifa ya siku mbili kwa washiriki kuhuu usikilizwaji wa kesi; na
(o) kuchukua hatua nyingine au kutoa amri nyingine, ikiwemo kubadili au kutengua amri kwa lengo la usimamizi wa kesi na kufanikisha lililopewa kipaumbele.

Mambo ya kuingizwa katika jalada la kesi ya jinai

**17**. Jalada la kesi ya jinai lililofunguliwa dhidi ya mtoto litajumuisha taarifa zilizoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

Mambo ya kuingizwa katika jalada la shauri la madai

**18**. Jalada la shauri la madai lililofunguliwa kuhusiana na mwenendo wa madai yanaomhusu mtoto litajumuisha taarifa zilizoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

Kupata na uchambuzi wa kumbukumbu za Mahakama

**19**.-(1) Mtoto au mwakilishi wake watakuwa na haki ya kupata kumbukumbu za Mahakama kuhusiana na kesi ya mtoto bila gharama yoyote.

(2) Nakala yoyote iliyoko kwenye jalada au nyaraka kuhusiana na kesi ya jinai iliyoko Mahakamani itatolewa bila gharama yoyote kwa mtoto anaye- shtakiwa na kwa mwakilishi wake atakapoomba.

(3) Nakala yoyote iliyoko kwenye jalada au nyaraka kuhusiana na kesi ya madai Mahakamani itakapohitajika itatolewa bila gharama yoyote kwa wahusika wa shauri.

## SEHEMU YA NNE
### KUFUNGWA KWA KESI YA JINAI DHIDI YA MTOTO

Mwenendo wa Mahakama

**20.** Mwenendo ulioainishwa chini ya Sehemu hii utatumika Mahakamani katika mashauri ya jinai.

Kutolewa kwa hati ya wito

**21**.-(1) Pale ambapo uamuzi umefanyika ya kumshtaki kwa kosa la jinai mtoto aliyepewa dhamana ya polisi, mtoto huyo atapewa hati ya wito wa kufika Mahakamani.

(2) Kila hati ya wito itatolewa na Mahakama na itakuwa kwa maandishi, katika nakala mbili, itasainiwa na kugongwa muhuri wa Mahakama.

(3) Kila hati ya wito itamtaka mtoto kuhudhuria Mahakamani katika muda na mahala palipoelekezwa.

(4) Pale ambapo mtoto yuko katika uangalizi wa mamlaka ya Serikali za mitaa, hati ya wito itakabidhiwa kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii wa mamlaka hiyo.

(5) Hati ya mashtaka, maelezo ya kosa na maelezo yoyote yanayotolewa na mtoto yatajumuishwa katika hati ya wito.

Kukamatwa kwa mtoto

**22**.-(1) Mtoto hatakamatwa, kuitwa au kuletwa mbele ya Mahakama isipokuwa kwa lengo la-

(a) kujibu malalamiko au shtaka dhidi yake; au
(b) kuwasilisha maombi ya kumweka rumande.

Hati ya ukamataji

**23**.-(1) Pale ambapo mtoto atashindwa kufika Mahakamani kuitikia wito, Mahakama inaweza kutoa hati ya mtoto huyo kukamatwa.

(2) Hati ya kukamatwa haitatolewa chini ya kanuni hii isipokuwa kama malalamiko yametolewa kwa kiapo na afisa wa polisi na-

(a) jitihada za kuwasiliana na mtoto baada ya kushindwa kuitikia wito wa kwanza zimefanyika bila mafanikio;
(b) mtoto hawezi kufikiwa au kupatikana;
(c) wito wa pili wa mtoto kuhudhuria Mahakamani umefanyika na mtoto ameshindwa kuitikia wito huo.

(3) Pale ambapo mtoto amekamatwa kwa hati ya kukamatwa, mtu aliyemkamata mtoto atamfahamisha na kumjulisha mzazi, mlezi, mwangalizi na mkuu wa idara ya ustawi wa jamii wa wilaya ambayo mtoto amekamatwa, juu ya-

(a) kukamatwa kwa mtoto;
(b) sababu ya kukamatwa; na
(c) mahali mtoto alipo.

(4) Pale ambapo mtoto amekamatwa kwa hati ya kukamatwa, mtoto huyo atapelekwa Mahakamani siku aliyokamatwa, na si zaidi ya siku inayofuatia baada ya kukamatwa kwake, isipokuwa kama kosa ni kubwa, na-

(a) mtoto anapokamatwa siku ya ijumaa baada ya saa za kazi, mtoto huyo anaweza kushikiliwa kizuizini mpaka siku ya jumatatu asubuhi; au
(b) mtoto anapokamatwa baada ya saa za kazi siku moja kabla ya siku ya mapumziko, mtoto huyo atafikishwa Mahakamani siku inayofuata ya kazi.

(5) Pale ambapo haiwezekani kumfikisha mtoto Mahakamani ndani ya saa ishirini na nne kama ilivyoelezwa katika kanuni ndogo ya (4)-

(a) polisi wataijulisha idara ya ustawi wa jamii ya eneo ambalo mtoto amekamatwa;na
(b) idara ya ustawi wa jamii itashirikiana na polisi kumweka mtoto katika makao yaliyothibitishwa au taasisi au kwa mtu mwenye uwezo mpaka mtoto huyo atakapofikishwa Mahakamani.

(6) Endapo mtoto atashikiliwa usiku mzima kwenye kituo cha polisi kwa hati ya kukamatwa, mtoto huyo atapewa chakula na maji ya kutosha, kitanda na mwanga na atawekwa katika chumba tofauti na chumba cha watu wazima.

(7) Hati ya kukamatwa itaandelea kuwa halali mpaka pale itakapotekelezwa au kufutwa.

Hati ya mashitaka

**24**.-(1) Hati ya mashtaka itajumuisha maelezo ya kosa mahsusi au makosa ambayo mtoto anatuhumiwa, pamoja na maelezo mengine muhimu ili kutoa taarifa za msingi kuhusu aina ya kosa analoshtakiwa.

(2) Mahakama, kabla ya kuanza kusikiliza kesi, itahakikisha upande wa mashtaka unampa mtoto au mwakilishi wa mtoto au idara ya ustawi wa jamii nakala ya hati ya mashtaka kwa wakati ili mtoto aweze kuandaa utetezi wake.

(3) Pale ambapo mtoto haelewi lugha ya Kiingereza au Kiswahili, Mahakama itahakikisha kuwa hati ya mashitaka na maelezo ya mashtaka yanatafsiriwa katika lugha inayoeleweka kwa mtoto.

Mahudhurio ya wazazi, walezi au waangalizi

**25**.-(1) Pale ambapo mzazi, mlezi, au mwangalizi aliye na taarifa ya shauri la mtoto kashindwa kuhudhuria katika shauri la jinai linalomhusu mtoto huyo, Mahakama inaweza kutoa hati ya wito kumtaka mzazi, mlezi au mwangalizi kuhudhuria Mahakamani kwa muda uliopangwa, isipokuwa kama-

(a) haitakuwa kwa maslahi ya mtoto, mzazi, mlezi au mwangalizi kuhudhuria;

(b) haiwezekani kwa mzazi, mlezi au mwangalizi kuhudhuria.

(2) Ikiwa mzazi, mlezi au mwangalizi aliyepokea wito kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) kashindwa bila sababu ya msingi kuhudhuri Mahakamani, Mahakama inaweza kutoa wito mtu huyo aletwe Mahakamani katika muda na mahali kama itavyoelekezwa katika hati hiyo.

(3) Ikiwa Mahakama itajiridhisha kwa ushahidi wa kiapo kwamba mzazi, mlezi au mwangalizi hawezi kuhudhuria shauri Mahakamani linalomhusu mwanawe isipokuwa mpaka kwa shinikizo, Mahakama hiyo inaweza kutoa hati ya kukamatwa na kumfikisha shahidi mbele ya Mahakama katika muda na mahala patakapo ainishwa katika hati hiyo ya kukamatwa.

(4) Pale ambapo wazazi, walezi au waangalizi hawakufahamishwa ndani ya muda wa kutosha kuweza kuhudhuria, au wameshindwa kuhudhuria kwa sababu za msingi, Mahakama, kwa dhumuni la kuhakikisha haki inatendeka, inaweza kutengua maamuzi au amri yoyote.

(5) Pale ambapo mtoto yuko katika uangalizi wa mamlaka ya serikali za mitaa, afisa ustawi wa jamii aliyepewa jukumu atahudhuria usikilizwaji wa shauri na atakuwa na haki sawa na mzazi.

Mzazi, mlezi au mwangalizi

**26**. Hakimu hatamuidhinisha mzazi,mlezi au mwangalizi kumsaidia mtoto katika mwenendo wa kesi yake iwapo atajiridhisha kwamba-

(a) mzazi, mlezi au mwangalizi huyo ameshtakiwa kwa kosa linalohusiana na maelezo yale yale ya kosa;

(b) mzazi, mlezi au mwangalizi amehukumiwa kwa kosa dhidi ya mtoto huyo;

(c) si kwa maslahi ya mtoto kupewa huduma hiyo; au

(d) mtoto huyo yuko katika uangalizi wa mamlaka ya serikali za mitaa na mamlaka hiyo ya serikali za

T.S. No. 11 la mwaka 2015

mitaa, katika kutekeleza haki yake ya malezi chini ya Kanuni za Usalama wa Mtoto, 2015 imeamua kuwa haitakuwa ni kwa maslahi ya mtoto, mzazi, mlezi au mwangalizi kumsaidia mtoto.

Shauri kutoendeshwa bila uwakilishi wa mtoto

**27.-**(1) Mahakama itahakikisha kuwa mtoto anawakilishwa katika usikilizwaji wa mashauri yote.

(2) Pale ambapo mtoto hana uwakilishi, hakimu ataahirisha shauri wakati wa usikilizwaji wa mwanzo kuruhusu mwakilishi kuteuliwa na mtoto kukutana na kuzungumza na mwakilishi wake.

(3) Ahirisho linalototolewa chini ya kanuni ndogo ya (2) halitazidi siku kumi na nne.

(4) Pale ambapo mwakilishi wa mtoto atakuwepo Mahakamani siku ya usikilizwaji wa kesi, kesi hiyo itaahirishwa kwa muda mfupi ili kutoa fursa kwa mtoto kuongea na mwakilishi na usikilizwaji wa kesi utaendelea siku hivyo.

Dhamana

**28.-**(1) Mtoto anayefika au kufikishwa Mahakamani kwa madhumuni ya usikilizaji wa shtaka lolote dhidi yake, isipokuwa kama kosa ambalo mtoto anashtakiwa halina dhamana, atapewa dhamana na kuwekwa katika uangalizi wa mzazi, mlezi, mtu anayefaa, taasisi inayofaa au kwa kamishna wa ustawi wa jamii na kurudishwa Mahakamani katika tarehe itakayotajwa.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni hii, endapo mtoto amewekwa chini ya uangalizi wa Kamishna wa Ustawi wa Jamii, uangalizi wa mtoto utakasimishwa kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii wa wilaya ambayo mtoto anaishi, na iwapo mtoto hana makazi maalum, uangalizi utakasimishwa kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii wa wilaya ambayo mtoto alikamatwa au katika idara nyingine ya ustawi wa jamii kwa kadri kamishna atakavyoona inafaa,

Isipokuwa kwamba iwapo mamlaka ya serikali za mitaa imechukua jukumu la huyo mtoto, mamlaka hiyo ya serikali za mitaa itaendelea kumtunza mtoto huyo kwa niaba ya Kamishna.

(3) Mtoto yeyote aliyetolewa kwa dhamana na kuwekwa chini ya usimamizi wa Kamishna atachukuliwa kama vile alikuwa mtoto anayerejewa chini ya Kifungu cha 94(5) cha Sheria.

(4) Mahakama inapomwachia mtoto kwa dhamana haitahitaji udhamini wa kifedha.

Kuwekwa mahabusi

**29.-**(1) Pale ambapo maombi ya kutiwa mahabusu yatafanyika dhidi ya mtoto aliyeshtakiwa kwa kosa lenye fursa ya dhamana, Mahakama itazingatia kwamba-

(a) dhamana haitakataliwa katika hali ambayo hakuna uwezekano wa mtoto kuhukumiwa kifungo cha jela; na

(b) kunyimwa fursa ya kuwa huru wakati kesi ikisubiriwa kuendelea kutatumika katika mazingira mahsusi kama hatua ya mwisho na kwa muda mfupi iwezekanavyo.

(2) Amri ya kumtia mtoto mahabusi itatolewa pale inapobidi na-

(a) pale ambapo mtoto au watu wengine walio katika hali ya hatari dhahiri;

(b) katika kipindi kilichotangulia mtoto alishindwa kuhudhuria Mahakamani kwa shtaka la jinai; au

(c) mtoto aliwahi kupewa dhamana na Mahakama na akashindwa kutii masharti ya dhamana au akatoroka.

(3) Hakimu, kabla ya kutoa amri ya mtoto kutiwa katika mahabusu ya watoto au eneo jingine la kizuizi kama ilivyoainishwa katika Fomu ya JRC Na.3, atazingatia iwapo mazingira mbadala yatakidhi kumsaidia mtoto na umma, kama vile-

(a) kumweka mtoto katika makazi chini ya uangalizi wa mzazi;

(b) kumkabidhi mtoto kwa mlezi, ndugu, rafiki wa familia, mtu anayefaa au taasisi inayofaa; au

(c) kumweka mtoto katika malezi ya Kamishna.

(4) Mtoto anayewekwa chini ya ulezi unaorejewa katika kanuni ndogo ya (3) atabaki katika ulezi huo mpaka maamuzi ya mwisho ya kesi isipokuwa pale ambapo Mahakama itakapoona inafaa kufanya mapitio ya maamuzi yake.

(5) Wakati wa kumweka mtoto chini ya uangalizi wa mtu anayefaa au taasisi inayofaa, Mahakama itazingatia umuhimu wa eneo la kumweka mtoto awe karibu zaidi na sehemu ya makazi ya kudumu ya wazazi au walezi kwa kadri itakavyowezekana kufanya hivyo.

(6) Kukosekana kwa malezi ya mzazi au makazi ya kudumu hakutakuwa ni sababu ya kumtia mtoto mahabusu.

(7) Mahakama wakati wa kumweka mtoto chini ya uangalizi, inaweza kuweka masharti na vigezo, ikiwemo -

(a) kumkataza mtoto kutembelea maeneo fulani au makazi;
(b) kumkataza mtoto kukutana na watu waliotajwa au makundi ya watu;
(c) kumtaka mtoto kubaki katika maeneo ya makaazi yake katika muda ulioainishwa;
(d) kumtaka mtoto kuhudhuria sehemu iliyotajwa na kama itaonekana inafaa, kwa muda uliotajwa ikiwemo shule;
(e) masharti mengineyo ambayo Mahakama itaona yanafaa kutolewa.

(8) Mahakama itakayoamua kumtia mtoto mahabusi, itatoa kipaumbele cha kumweka mtoto katika mahabusu ya watoto inayohifadhi watoto wa umri wa chini ya miaka kumi na nane.

(9) Pale ambapo mtoto atatiwa mahabusi, mtoto huyo atatengwa na watu wazima, atapewa uangalizi na kinga na mahitaji binafsi muhimu ya kijamii, elimu, ufundi, kisaikolojia, kitabibu na msaada wa kimwili atakaouhitaji kulingana na umri wake, jinsia, ulemavu, hali ya afya na mazingira mengine binafsi.

Tathmini ya awali ya mtoto

**30.**-(1) Mtoto yeyote aliyetiwa mahabusi atafanyiwa tathmini na afisa ustawi wa jamii ndani ya siku tatu tangu kutiwa mahabusi.

(2) Ripoti ya maandishi ya tathmini itawasilishwa katika Mahakama ya watoto si zaidi ya siku mbili kabla ya mapitio ya muhula wa kwanza wa mtoto kuwa mahabusu.

(3) Pale itakapowezekana, taarifa ya tathmini itajumuisha taarifa zifuatazo-

(a) taaarifa za familia ya mtoto na maelezo mengine muhimu kuhusu mtoto ambayo yanaweza kuisaidia Mahakama ya mtoto;
(b) iwapo mtoto atahitaji malezi na ulinzi chini ya Sehemu ya Tatu ya Sheria;
(c) kadirio la umri wa mtoto kama umri wake haufahamiki;

(d) mapendekezo kuhusu mtoto kuachiwa huru kutoka mahabusu na hifadhi mbadala ya mtoto kwa kipindi ambacho anasubiri kesi kuanza;

(e) mambo yoyote yanayoweza kuathiri uwezekano wa mtoto kutenda kosa la jinai; na

(f) taarifa zozote nyingine muhimu kuhusiana na mtoto ambazo afisa ustawi wa jamii anaona ni za muhimu na ambazo zitafanikisha lengo la sheria.

(4) Afisa ustawi wa jamii atatakiwa kuwepo wakati wa shauri la mapitio Mahakamani na, itakapohitajika na Mahakama, atatoa ushahidi kwa jambo lolote lililomo katika taarifa hiyo.

Mapitio ya amri ya mahabusu

**31**.-(1) Amri ya kuwekwa mahabusi itafanyiwa mapitio kila baada ya siku kumi na nne.

(2) Mtoto atatakiwa kuwepo kila wakati wa kufanya mapitio ya amri ya kuwekwa mahabusi.

(3) Mahakama itazingatia taarifa ya kwanza ya tathmini ya afisa ustawi wa jamii na kutathmini kama mtoto anaweza kutoka kwa dhamana au kuendelea kubaki mahabusi.

(4) Pale ambapo mtoto atafuata vigezo vilivyoainishwa chini ya kanuni ya 29(2) na ikishindikana kumweka mahala popote palipo na ulezi paliporejewa chini ya Kanuni ya 29(3), Mahakama itaongeza muda wa kuwekwa mahabusi.

(5) Mahakama itakapoona kwamba mtoto haoneshi tena hali ya hatari kwake mwenyewe au kwa mtu yeyote mwingine, na hahusiki na masharti ya kanuni ya 29(2)(b), itamtoa mtoto huyo kwa dhamana.

(6) Pale ambapo taarifa ya tathmini ya kwanza inapendekeza kuwa kesi inafaa kwa ajili ya adhabu nafuu, hakimu atamwalika mwendesha mashtaka kuielezea Mahakama uhitaji wa kuendelea kumweka mtoto mahabusi na inaweza kumuelekeza mwendesha mashtaka kutathimini adhabu nafuu ya mtoto.

(7) Pale ambapo mtoto hana makazi yoyote ambayo anaweza kurejea baada ya kuachiwa kutoka kwenye mahabusi amri ya ulinzi wa mtoto kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii katika wilaya ambayo mtoto ana makazi au kama mtoto hana makazi ya kudumu, kwa wilaya ambayo mtoto alikamatwa au wilaya ambayo Mahakama ilipo, isipokuwa kama mamlaka nyingine ya serikali za mitaa imekwishachukua jukumu la mtoto, mamlaka hiyo itaendelea na jukumu hilo.

(8) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (7), Mahakama inaweza kutathmini kwamba mamlaka ya serikali za mitaa imekwishachukua jukumu la mtoto kama afisa ustawi wa jamii anayeandaa taarifa ya tathmini amempata mbadala anayefaa kwa ajili ya mtoto katika wilaya hiyo na mamlaka ya serikali za mitaa husika imekubali kuchukua jukumu la mtoto.

(9) Mtoto anaerejewa katika kanuni ndogo ya (7) atapatiwa makazi na kusaidiwa na idara ya ustawi wa jamii kwa mujibu wa kifungu cha 94(5) cha sheria.

(10) Mahakama-

(a) itarekodi na kutoa sababu za kuongezewa kwa amri ya mahabusu au uamuzi wa kumuachia mtoto kwa dhamana; na

(b) itampatia mwakilishi wa mtoto nakala ya rekodi.

(11) Kwa madhumuni ya kanuni hii, adhabu nafuu ina maana mfumo wa kutoa fursa kwa mkosaji wa jinai wa mara ya kwanza kuhusiana na makosa madogo madogo, kutumikia adhabu ya huduma za jamii, kufidia hasara kutokana na kosa, kupata tiba ya ulevi au utumiaji madawa au ushauri nasaa kwa kufanya matendo yasiyofaa katika jamii au tabia zitokanazo na utindio wa akili, na endapo mshtakiwa huyo atatoa ushirikiano na mpango wa unafuu ukaonesha mafanikio, Mahakama inaweza kutathimini mahabusu kwa mujibu wa kanuni hii.

## SEHEMU YA TANO
### Kesi ya Jinai Dhidi ya Mtoto

kujibu shtaka

**32.**-(1) Pale ambapo mtoto ameshtakiwa kwa kosa, Mahakama itamfafanulia mtoto katika lugha anayoielewa-

(a) msingi wa shtaka na maelezo ya kosa;

(b) maelezo yatakayo hitaji kuthibitishwa kabla mtoto hajapatikana na hatia;

(c) jukumu la hakimu; na

(d) taratibu za Mahakama.

(2) Mtoto ataambiwa ajibu shtaka baada ya kupewa fursa ya kukutana na mwakilishi wake.

(3) Mtoto akikiri shtaka, Mahakama itarekodi, kwa ufasaha iwezekanavyo, matamshi aliyoyatumia kukiri na itarekodi kuwa amekiri shtaka.

(4) Mahakama itamwalika mwendesha mashtaka kuwasilisha muhtasari wa ushahidi na kumtaka mtoto kujibu maelezo.

(5) Pale ambapo Mahakama itaridhika kwamba majibu ya maelezo yanapelekea kukiri dhahiri kwa shtaka, itatoa hukumu na baada ya kukamilika kwa taarifa ya uchunguzi wa kijamii, itatoa adhabu kwa mujibu wa kanuni ya 48.

(6) kama majibu ya mtoto chini ya kanuni hii hayapelekei kukiri dhahiri kwa shtaka,Mahakama itarekodi kukana kwa shtaka.

Pale ambapo mshitakiwa anakubali kosa

**33**. Pale ambapo mtoto anakana shtaka kwa kosa ambalo anashtakiwa au iwapo Mahakama haijakubaliana na kukiri kwa shtaka kwa mtoto, Mahakama-

(a) itarekodi kukana kwa shtaka;
(b) itaweka sahihi chini ya maelezo yaliyorekodiwa; na
(c) itaendelea kusikiliza ushahidi wa upande wa mashtaka.

Muda wa kuendeshwa kwa kesi ya jinai

**34**.-(1) Kesi yoyote ya jinai inayoendeshwa na Mahakama itakamilika ndani ya miezi sita baada ya mtoto kufikishwa kwa mara ya kwanza Mahakamani kwa shtaka linalomkabili.

(2) Baada ya muda uliotajwa katika kanuni ndogo ya (1) kwisha, Mahakama, kwa sababu njema ambazo zitarekodiwa, inaweza kuongeza muda wa kukamilika kwa kesi kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu.

Ushiriki wa mtoto katika mwenendo

**35**.-(1) Mahakama itakapoona kwamba mtoto aliyeshtakiwa hawezi kushiriki katika shauri kutokana na kutolielewa shauri, au hana uwezo wa kumwelekeza wakili, mlezi au mwakilishi wake kuhusiana na utetezi wake, Mahakama itasitisha kuendesha mashauri kwa siku saba ili kuamua iwapo usikilizwaji unaozingatia usawa unaweza kuzingatiwa.

(2) Katika kutathmini kama usikilizwaji unaozingatia usawa unaweza kuzingatiwa, Mahakama inaweza kumtaka afisa ustawi wa jamii kumhoji mtoto na kurejesha taarifa Mahakamani kuhusu uwezo wa mtoto kushiriki kulielewa shauri.

(3) Mahakama itakaporidhika kuwa mtoto hawezi kushiriki au kulielewa shauri, kufanya utetezi au kumuelekeza wakili wake, mlezi wa kuteuliwa na Mahakama au mwakilishi mwingine kuhusiana na utetezi wake, itafuta shtaka na kuelekeza

mtoto afikishwe kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii aliyoko-

(a) katika wilaya ambayo mtoto anaishi;

(b) katika wilaya ambayo mtoto alikamatwa au Wilaya ambayo Mahakama husika ipo;au

(c) iwapo mamlaka nyingine ya serikali za mitaa imekwishachukua jukumu la mtoto huyo, katika mamlaka hiyo,

ili kuamua kama shauri kuhusu kinga ya mtoto lifunguliwe.

(4) Pale ambapo mtoto ameachiwa huru na Mahakama kwa sababu zozote zile na anahusishwa na kifungu cha 94(5) cha Sheria kuwa mtoto huyo-

(a) kapotea, katelekezwa au anatafuta hifadhi; na

(b) anahitaji msaada na malazi,

mtoto atakabidhiwa kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii wa Wilaya ambayo mtoto anaishi, au kama mtoto hana makazi maalum, kwa wilaya ambayo mtoto alikamatwa au Wilaya ambayo Mahakama ipo, au iwapo mamlaka nyingine ya serikali za mitaa imekwishachukua jukumu la mtoto,kwa mamlaka hiyo.

(5) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (3) na (4), Mahakama inaweza kuchukulia mamlaka ya serikali za mitaa imekwishachukua jukumu la mtoto kama afisa ustawi wa jamii amepata mbadala unaofaa wa malezi ya mtoto katika wilaya hiyo na mamlaka ya serikali za mitaa hiyo imekubali kuchukua jukumu la mtoto.

Jukumu la kuweka wazi kesi ya upande wa mashitaka

**36**.-(1) Mwendesha mashtaka atawasilisha Mahakamani maelezo yaliyodurufiwa ya taarifa ya upande wa mashtaka kabla ya usikilizwaji wa awali wa kesi.

(2) Mahakama itampatia mtoto au mwakilishi wake nakala ya maelezo ya upande wa mashtaka kabla ya kesi kuanza kusikilizwa kwa mara ya kwanza.

(3) Maelezo ya upande wa mashtaka yatajumuisha-

(a) hati ya mashtaka na ufafanuzi wa kosa;

(b) maelezo ya kosa;

(c) nyaraka yoyote au sehemu iliyoziduliwa ambayo ndiyo itakuwa msingi wa kesi; na

(d) hukumu yoyote ya nyuma dhidi ya mtoto.

(4) Mwendesha mashtaka, ndani ya siku kumi na nne kabla ya mwenendo wa mwisho wa mashauri, atawasilisha Mahakamani maelezo yoyote ya mashahidi na ushahidi mwingine

wowote anaotarajia kuutumia.

(5) Mwendesha mashtaka, wakati shauri linaendelea, atafanya mapitio ili kubaini kama kuna taarifa za uendeshaji mashtaka zinazoweza kudhoofisha kesi ya upande wa mashtaka dhidi ya mtoto au zinazoweza kusaidia kesi upande wa mtoto, ambazo hazijawahi kutolewa Mahakamani.

(6) Pale ambapo mwendesha mashtaka atapata taarifa zilizotajwa chini ya kanuni ndogo ya (5) wakati wowote ambao shauri linaendelea, mwendesha mashtaka atazitoa taarifa hizo Mahakamani.

(7) Taarifa za mwendesha mashtaka zinajumuisha taarifa-

(a) zilizoko katika dhamana ya mwendesha mashtaka na zilizofika katika dhamana yake kupitia kesi ya upande wa mashtaka dhidi ya mshtakiwa; au

(b) ambazo amezikagua kuhusiana na kesi upande wa mwendesha mashtaka dhidi ya mshitakiwa.

(8) Pale ambapo upande wa mashtaka utashindwa kuwasilisha maelezo ya upande wa mashtaka katika muda unaotakiwa, Mahakama, kwa maombi ya mshitakiwa au kwa hiari yake yenyewe, itauamuru upande wa mashtaka kuwasilisha nyaraka husika ndani ya siku tatu.

(9) Mahakama, kabla haijatekeleza mamlaka yake chini ya kanuni ndogo ya (8), itaupa upande wa mashtaka haki ya kujieleza kuhusu kushindwa kwake kutoa maelezo**.**

Usikilizwaji wa awali

**37**.-(1) Pale ambapo mtoto anayeshitakiwa amekana shitaka dhidi yake, hakimu anayeendesha shauri atapanga tarehe ya usikilizwaji wa awali na tarehe hiyo itakuwa ndani ya siku kumi na nne tangu siku ambayo shtaka liliposomwa.

(2) Usikilizwaji wa awali wa shauri unaweza kufanyika wakati wa usikilizwaji wa kwanza wa shauri iwapo mtoto ana mwakilishi.

(3) hakimu atamfafanulia mtoto na mwakilishi wake namna, na dhumuni la usikilizwaji wa awali wa shauri.

(4) Mwendesha mashtaka atasoma maelezo ya shitaka kwa mshitakiwa wakati wa usikilizwaji wa awali, katika lugha ambayo mtoto anaielewa, au iwapo mtoto haelewi Kiswahilii au Kiingereza, mbele ya mkalimani aliyeteuliwa kwa ajili ya mtoto.

(5) Wahusika katika shauri, baada ya kusomewa maelezo ya shtaka, watakubaliana juu ya mambo yasiyobishaniwa.

(6) Hakimu anaweza kuuliza maswali au kuomba

ufafanuzi kuhusiana na maelezo ya shtaka na majibu kuhusiana na maswali hayo yanaweza kutolewa bila kiapo au uthibitisho.

(7) Wakati wa ukamilishaji wa usikilizwaji wa awali, Mahakama itaandaa hati ya mambo yaliyokubalika na hati hiyo itasomwa na kufafanuliwa kwa mtoto katika lugha ambayo mtoto huyo anaielewa,na itasainiwa na afisa anayeendesha shauri, mtoto, Wawakilishi wa mtoto na mwendesha mashtaka, na kisha kuwasilishwa Mahakamani.

(8) Maelezo yoyote au nyaraka zilizopokelewa au kukubaliwa katika hati iliyowasilishwa chini ya kanuni ndogo ya (7), zitachukuliwa kuwa zimethibitika rasmi:

Isipokuwa kwamba, iwapo wakati shauri likiendelea Mahakama itakuwa na mtazamo kuwa maslahi ya kutendeka kwa haki yanahitaji hivyo, Mahakama inaweza kuelekeza maelezo yoyote au nyaraka zilizopokelewa au kukubaliwa katika hati iliyowasilishwa chini ya kanuni hii ndogo zithibitishwe rasmi.

(9) Mashahidi hawataitwa wakati wa usikilizwaji wa awali.

(10) Mahakama inaweza kutoa taarifa kwa mtu yeyote ambaye anaweza kuitwa kama shahidi baada ya usikilizwaji wa awali, kwamba anaweza kuhitajika kutoa ushahidi Mahakamani katika tarehe itakayotajwa kwenye taarifa na taarifa hiyo itachukuliwa kuwa ni wito uliotolewa na kukabidhiwa kwa mtu huyo kufika na kutoa ushahidi.

(11) Hakimu anayehusika na usikilizwaji wa mwanzo wa shauri atahusika na usikilizwaji wa mashauri yanayofuatia kuhusiana na shtaka dhidi ya mtoto, isipokuwa kama itakuwa nje ya uwezo wake kufanya hivyo, au itasababisha ucheleweshaji usio stahili.

Ahirisho linalotokana kutohudhuria kwa wahusika au mashahidi

**38**.-(1) Pale ambapo mwendesha mashtaka anashindwa kuhudhuria Mahakamani kwa siku iliyopangwa kwa ajili ya usikilizwaji na hajaitaarifu Mahakama kuhusu kushindwa kwake kuhudhuria, Mahakama itapanga tarehe nyingine, na kumtaarifu mwendesha mashtaka kuhusu kushindwa kwake kuhudhuria.

(2) Pale ambapo mwendesha mashtaka atashindwa kuhudhuria Mahakamani katika tarehe nyingine ya usikilizwaji iliyopangwa na hajaitaarifu Mahakama kushindwa kwake kuhudhuria, kesi itafutwa.

(3) Endapo afisa ustawi wa jamii anayehusika na taarifa ya tathmini ya kwanza au taarifa ya uchunguzi wa kijamii,

atashindwa kuhudhuria siku iliyopangwa, na hajaitaarifu Mahakama kuhusu kushindwa kwake kuhudhuria, Mahakama itatoa wito kwa afisa huyo au mkuu wa idara ya ustawi wa jamii kutoa maelezo ya kushindwa kuhudhuria.

(4) Pale ambapo shahidi wa upande wa mashtaka, akiwemo shahidi ambaye ni mtoto au shahidi wa utetezi watashindwa kuhudhuria Mahakamani bila sababu ya msingi, kuitikia wito Mahakama-

(a) itaachana na shahidi huyo na kuendelea na shauri; au

(b) itatoa amri ya mtu huyo kufikishwa Mahakamani katika muda na mahala patakapoainishwa kwenye amri.

(5) Mahakama, mara shauri litakapoanza,itaendelea kusikiliza mashahidi katika kesi bila kuahirisha kesi au kusikiliza sehemu ya shauri;

Isipokuwa kwamba, iwapo shahidi ana sababu za msingi za kushindwa kuhudhuria, Mahakama inaweza kuahirisha ili kuruhusu ushahidi wa shahidi kusikilizwa au maamuzi mengine kufanyika kwa kadri itakavyoona inafaa.

(6) Pale ambapo maamuzi ya kuahirisha kesi yatatolewa baada ya kesi kuanza kusikilizwa na kesi ikasikilizwa nusu, Mahakama itaendelea na usikilizwaji wa kesi kwa tarehe ya karibu zaidi itakayopangwa.

Ushahidi wa upande wa mashtaka

**39**.-(1) Mara baada ya upande wa mashtaka kumaliza kutoa maelezo na ushahidi wa mashtaka, Mahakama itaamua kama kuna shtaka la kujibu na mtoto ana kesi ya kujibu.

(2) Pale ambapo Mahakama itaamua kwamba upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha kesi yake kikamilifu kuhitaji mtoto kujibu shtaka, itafuta shtaka na kumwachia huru mtoto.

(3) Pale ambapo upande wa mashtaka umethibitisha kuwa ipo kesi ya kujibu, Mahakama itasikiliza mashahidi wa upande wa utetezi na maelezo yoyote ya nyongeza ambayo mtoto atahitaji kuyatoa katika utetezi wake.

Kupokelewa kwa ushahidi wa kitabibu

**40**.-(1) Pale ambapo taarifa ya kitabibu inataka kutolewa kama ushahidi katika kesi, upande wa mashtaka na utetezi, wakati wa, au kabla ya usikilizwaji wa awali, watashauriana kuhusu mambo watakayokubaliana katika ushahidi huo wa kitabibu.

(2) Pale ambapo maelezo yaliyomo katika taarifa ya kitabibu yamekubalika, taarifa hiyo ya kitabibu inaweza

kuwasilishwa Mahakamani na afisa tabibu aliye mhudumia mtu ambaye ni muhusika wa taarifa ya kitabibu hataitwa kutoa ushahidi.

(3) Pale ambapo afisa tabibu aliyemchunguza mtu ambaye ni muhusika wa taarifa ya kitabibu hapatikani kama shahidi, afisa tabibu mwingine anaweza kuitwa kuthibitisha maelezo katika taarifa ya kitabibu.

Kupokelewa kwa ushahidi wa maungamo Sura ya 6

**41**.-(1) Ushahidi wowote wa maungamo unaotolewa na mtoto kwa hiari mbele ya askari polisi kwa mujibu wa Sheria ya Ushahidi, kwa kosa aliloshtakiwa, unaweza kupokelewa na Mahakama ya watoto kama ushahidi.

(2) Jukumu la kuthibitisha kuwa maungamo ya mtoto anayeshtakiwa yametolewa kwa hiari liko kwa upande wa mashtaka.

(3) Mahakama, katika kuamua kama maungamo yalitolewa kwa hiari, itatilia maanani umri wa mtoto, maendeleo ya mtoto, muda uliotumika katika kumhoji mtoto, uelewa wa mtoto, hofu ya madhara yasiyojulikana au ya uwezekano wa kifungo, kama kuna ushawishi wowote uliotolewa, na kama mzazi, mlezi, mwangalizi wa mtoto, mlezi wa kuteuliwa na Mahakama au mwakilishi wa kisheria alikuwepo kumsaidia mtoto.

(4) Mahakama ikifikia maamuzi kuwa ushahidi wa maungamo haukutolewa kwa hiari, haitapokea ushahidi huo.

Utetezi

**42.** Mtoto atafahamishwa kuwa ana haki ya-

(a) kutoa ushahidi kwa kiapo au bila kiapo; na

(b) kuita mashahidi kwa niaba yake.

Ushahidi mkuu wa mtoto mshtakiwa

**43.**-(1) Ushahidi mkuu utatolewa kwa mdomo.

(2) Mahakama, wakati wa usikilizwaji wa ushahidi mkuu wa mshtakiwa, itaendesha shauri katika hali isiyo rasmi iwezekanavyo na bila kutumia masharti makali ya utoaji ushahidi isipokuwa kama kufanya hivyo ni muhimu kwa maslahi ya mtoto.

Mamlaka ya Mahakama kuamuru utolewaji wa ushahidi

**44.** Mahakama, katika shauri lolote mbele yake, inaweza kufanya mahojiano na pande zote husika za shauri na mashahidi, na itakuwa na mamlaka ya kuamuru kutolewa au kuletwa Mahakamani ushahidi unaohitajika.

Udadisi wa mashahidi

**45**.-(1) Mtoto anayeshtakiwa anaweza kuulizwa maswali katika ushahidi wake na mwendesha mashtaka au mshtakiwa mwenzake.

(2) Shahidi, isipokuwa mshtakiwa, anaweza kuulizwa maswali katika ushahidi wake na mhusika yeyote katika shauri ispokuwa muhusika aliyeita shahidi, lakini sio shahidi anayetoa ushahidi unaokinzana.

(3) Mahakama itahakikisha kuwa udadisi unafanyika kwa utaratibu wa kumuongoza mtu na kwamba haki ya mtoto kuto kujifunga mwenyewe kwa maelezo yake itazingatiwa.

(4) Mtu anayeuliza maswali kwa mtoto anayeshtakiwa au shahidi ambaye ni mtoto-

(a) atatumia lugha rahisi ambayo mtoto anaweza kuielewa;

(b) atauliza maswali mafupi na ya moja kwa moja; na

(c) atajiepusha na malumbano, uonevu au kumfanyia ufedhuli mtoto.

(5) Mahakama, wakati wa usikilizwaji na kukamilika kwa ushahidi wa shahidi, inaweza kumuuliza shahidi maswali muhimu na inayoona yanafaa-

(a) kufafanua ushahidi;

(b) kwa madhumuni ya kuthibitisha ukweli wa maelezo yaliyotolewa; au

(c) kupima uaminifu wa shahidi.

(6) Mahakama itaongoza na kuelekeza utendaji wa pande zote za wahusika katika shauri kwa kudhibiti maswali yasiyo na umuhimu au kurudia kwa maswali kusikohitajika.

Mtoto kutiwa hatiani

**46**.-(1) Mahakama baada ya kusikiliza mashahidi, ikiridhika pasipo kuacha shaka kwamba kosa dhidi ya mtoto limethibitika, itamtia hatiani kwa kosa analoshtakiwa.

(2) Mtoto anaposhtakiwa kwa kosa linalohusisha maelezo mbalimbali yanayopelekea kosa dogo na kubwa**,** na maelezo yanayopelekea kosa dogo yakathibitika, Mahakama inaweza kumtia hatiani mtoto kwa kosa hilo dogo hata kama hakushitakiwa kwa kosa hilo.

(3) Mwendesha mashtaka ataifahamisha Mahakama kama mtoto ni mtendaji kosa wa mara ya kwanza au kama amekwishawahi kutenda kosa la jinai.

(4) Mahakama, baada ya kumtia hatiani mtoto na kabla ya kutoa hukumu, itamwelekeza afisa ustawi wa jamii wa Mahakama kuandaa taarifa ya uchunguzi wa kijamii, itakayowasilishwa Mahakamani ndani ya siku kumi na nne tangu siku ilipoelekezwa iandaliwe.

Taarifa ya uchunguzi wa kijamii kabla ya hukumu

**47**.-(1) Taarifa ya uchunguzi wa kijamii itajumuisha taarifa kuhusu mtoto, ambazo ni pamoja na-

(a) historia ya maisha ya mtoto na maelezo kuhusu mambo mengine ambayo yanaweza kuwa na msaada kwa Mahakama;

(b) hali ya familia ya mtoto kwa sasa, na hali ya mapitio ya maisha ya mtoto huyo akiwa nyumbani;

(c) iwapo mtoto anakwenda shule, anapata mafunzo yoyote au ameajiriwa;

(d) hali ya afya ya mtoto;

(e) makosa ya nyuma iwapo mtoto amewahi kutenda;

(f) tathmini ya uwezekano wa mtoto kurudia kosa au kusababisha madhara makubwa; na

(g) mapendekezo kuhusu hukumu stahiki kwa kutilia maanani kuwa dhumuni la kuhukumu litakuwa ni kumrudisha katika tabia njema na kumwezesha mtoto kuwa mbunifu katika familia yake na jumuiya.

(2) Taarifa ya uchunguzi wa kijamii itakuwa ya ukweli, bila upendeleo na isiyo bagua, penye mapendekezo yaliyo dhahiri na ya kupitisha hukumu dhidi ya mtoto.

(3) Afisa ustawi wa jamii, wakati wa uandaaji wa taarifa ya uchunguzi wa kijamii, atazingatia taarifa ya tathmini ya kwanza na kushauriana na wataalamu wengine ambao wamewahi kuwasiliana na mtoto.

(4) Mahakama itamwachia mtoto kwa dhamana wakati taarifa ya uchunguzi wa kijamii inaandaliwa na kabla ya hukumu kutolewa, isipokuwa kama vigezo vilivyomo katika kanuni ya 29(2) vimetekelezwa na si rahisi kuulinda umma kwa kuweka hiari na kutekeleza masharti yaliyomo katika kanuni ya 29(3) na (7).

Hukumu

**48.**-(1) Hakimu aliyesikiliza shauri atatoa hukumu kwa maandishi itakayojumuisha ushahidi uliowasilishwa na hoja zilizohitaji kuamuliwa, maamuzi na sababu za maamuzi.

(2) Hukumu inayotolewa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya

(1) itawekewa tarehe na saini ya Hakimu kwa siku ambayo ilisomwa Mahakamani.

(3) Endapo kwa sababu yoyote ile, Hakimu hawezi kusoma hukumu yake ya maandishi katika Mahakama kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), Mahakama itampangia hakimu mwingine kusoma hukumu Mahakamani.

(4) Hukumu zote zitasomwa katika Mahakama ndani ya siku ishirini na moja baada ya kukamilika kwa mwenendo wa shauri.

(5) Hukumu, ikiwa mtoto ametiwa hatiani, itabainisha kosa na kifungu cha kanuni za adhabu au sheria nyingine ambacho mshtakiwa ametiwa hatiani.

(6) Hukumu ikiwa hakuna hatia, itaeleza kosa ambalo mshtakiwa hakupatikana na hatia na itaelekeza kuwa mshtakwia huyo aachiwe huru.

(7) Mahakama itamuelezea mtoto kiini cha hukumu iliyotolewa na matokeo yake.

## SEHEMU YA SITA
### HUKUMU

Utaratibu wa kutoa hukumu

**49.-**(1) Mahakama, kabla ya kufikia maamuzi ya kutoa hukumu stahiki dhidi ya mtoto aliyetiwa hatiani, itaweka maanani misingi ifuatayo-

(a) uhitaji wa uwiano unaozingatia mazingira ya kosa na mkosaji.

(b) umuhimu wa kumrudisha mtoto mhalifu katika hali ya ubora na kumjumuisha;

(c) hoja ya kuendeleza na kukuza mahusiano ya kifamilia inapobidi;

(d) umuhimu wa kuweka vikwazo vyepesi kulingana na lengo halali la kuwalinda waathiriwa na jamii;

(e) umuhimu wa watoto wahalifu kukubali kuwajibika kutokana na matendo yao na tabia ya uwajibikaji kuwa na manufaa na kutenda matendo yanayokubalika kijamii.

(f) haja ya kuweka maanani masuala yaliyochangia mtoto kuwa na tabia ya kihalifu, ikiwemo matatizo ya kiakili au udhaifu wa kujifunza, ufukara, mafanikio hafifu ya elimu na kukosa malezi; na

(g) haja ya kuweka maanani mazingira maalum ya makundi

ya watoto wahalifu, hususan watoto waishio katika mazingira magumu.

(2) Mahakama, kabla ya kupitisha hukumu, itazingatia-

(a) taarifa ya uchunguzi wa kijamii;

(b) ombi lolote la kupunguza ukali wa adhabu lililotolewa na mtoto au lililotolewa kwa niaba yake;

(c) adhabu stahiki kwa mtoto na madhara aliyosababisha, aliyokusudia au aliyoyataraji, kwa kuzingatia mambo yanayokuza na kuweka unafuu wa adhabu;

(d) kwamba kuwekwa katika shule iliyothibitishwa kufanyike tu kama hatua ya kipekee, ya mwisho na kwa muda mfupi iwezekanavyo; na

(e) endapo kuachiwa huru au kifungo cha nje kitakuwa ni kwa maslahi ya mtoto na maslahi ya haki kutendeka.

Kuachiwa kwa masharti

**50.-**(1) Pale ambapo mtoto atatiwa hatiani kwa kosa, Mahakama inaweza kutoa amri ya kumwachia mhalifu kwa masharti baada ya kuweka ahadi mbele ya Mahakama ya kuwa na tabia njema kwa kipindi kitakachoainishwa ambacho hakizidi miaka mitatu.

(2) Mahakama inaweza kutaka udhamini wa mzazi au mlezi wa mtoto,

isipokuwa kwamba udhamini wa kifedha hautahitajika iwapo mzazi, mlezi mtoto hana uwezo wa kulipa.

(3) Mahakama inaweza kuweka masharti ikiwemo-

(a) kumweka mtoto chini ya usimamizi wa mzazi, mlezi ndugu au mkuu wa Idara ya Ustawi wa jamii kama atakavyotajwa katika amri; na

(b) masharti mengineyo ambayo Mahakama itaona yanafaa, ikiwemo lakini sio kwa ukomo-

(i) ombi la msamaha kwa mdomo au maandishi wa mtu, watu au taasisi husika;

(ii) kuhusishwa na programu ya jamii ya kujirekebisha au kujumuika;

(iii) mtoto kupelekwa kupata ushauri au matibabu;

(iv) urejeshaji wa vitu vilivyoainishwa kwa mwathirika aliyeorodheshwa au waathirika wa kosa iwapo kitu hicho kinaweza kurejeshwa kwa mhusika au kurudishwa katika hali ya kawaida;

(v) utoaji wa huduma au fidia fulani kwa

mwathirika au waathirika wa kosa, isipokuwa kwamba huduma ya aina hiyo itakuwa ni kwa mujibu wa Sehemu ya Saba ya Sheria;

(vi) iwapo hajatambulika mtu au watu ambao urekebishwaji au urejeshwaji unaweza kufanyiwa kwao, utoaji wa huduma au fidia kwa jamii; na

(vii) kuelekeza mtoto kupelekwa katika kongamano la kikundi cha familia au upatanishi wa muathiriwa na mkosaji.

(4) Mahakama itahakikisha kuwa-

(a) mzazi, mlezi au ndugu ambaye ametajwa kama msimamizi anaelewa majukumu ya usimamizi wa kuyakubali, majukumu hayo; na

(b) mtoto anaelewa na kukubali masharti yanayoambatana na maamuzi kutolewa kwa masharti.

(5) Pale ambapo maamuzi ya kutolewa kwa masharti pamoja na usimamizi yameonekana kwa Mahakama kuwa ni adhabu inayofaa kwa mtoto, lakini hakuna mzazi, mlezi au ndugu mwenye nia ya kumsimamia mtoto, Mahakama itamweka mtoto chini ya usimamizi wa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii wa wilaya ambayo mtoto anaishi, au kama mtoto haishi huko, au hana makazi maalum, wilaya ambayo mtoto alikamatwa au ambayo Mahakama ilipo, isipokua kama mamlaka ya serikali za mitaa imechukua jukumu la mtoto, itaendelea na jukumu hilo.

(6) Kwa madhumuni ya Kanuni ndogo ya (5), Mahakama inaweza kuchukulia kwamba mamlaka ya serikali za mitaa imekwishachukua jukumu la kumsimamia mtoto iwapo afisa ustawi wa jamii amepata mbadala unaofaa katika Wilaya kwa ajili ya mtoto na kwamba mamlaka ya serikali za mitaa imeamua kuchukua jukumu la kumsimamia mtoto huyo.

(7) Pale ambapo mtoto hana makazi maalumu au hana malezi, utaratibu wa kinga ya mtoto utafanywa na Idara ya Ustawi wa Jamii husika kwa mujibu wa Kanuni ndogo ya (5) na atamhifadhi na kumsaidia mtoto.

Faini, fidia na gharama

**51.-**(1) Faini, fidia au gharama zinaweza kuwekwa kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 118 cha Sheria, kufidia hasara iliyosababishwa na matendo ya mtoto.

(2) Mtoto ambaye ni muhusika wa amri ya kuwekwa chini ya uangalizi kama ilivyoainishwa katika Fomu ya JCR Na.13 ya

Jedwali ya Tatu la Kanuni hizi, anaweza kuhusishwa na masharti yoyote yafuatayo ambayo Mahakama inaona ni muhimu na sahihi kuyafanya:

(a) utoaji taarifa kwa afisa ustawi wa jamii katika muda na mahala husika;

(b) kuheshimu maelekezo yoyote ya afisa ustawiwa jamii;

(c) kutoa taarifa ya mabadiliko yoyote ya anuani, shule au ajira;

(d) kutoondoka katika eneo la makazi bila ruhusa;

(e) kuzuiliwa kuonana au kuwasiliana na mtu au watu waliotajwa;

(f) kuzuiliwa kuingia majengo yaliyotajwa au maeneo yaliyoainishwa;

(g) kuheshimu masharti ya shule au ya nyumbani.

(3) Pale ambapo Mahakama inakusudia kutoza faini, fidia au gharama dhidi ya mzazi, mlezi au ndugu, mtu huyo atapewa fursa ya kusikilizwa na Mahakama.

(4) Mahakama, wakati wa kutoa amri ya kutoza faini, fidia au gharama dhidi ya mzazi, mlezi au ndugu, itazingatia madhara ya amri hiyo kwa mwathirika, na mahusiano kati ya mtu aliyeamrishwa kulipa na mtoto.

Amri ya kuwekwa chini ya uangalizi

**52.-**(1) Mahakama itakapoona kuwa kuachiwa bila masharti mengine hakujitoshelezi itatoa amri ya kuwekwa chini ya uangalizi.

(2) Mtoto ambaye anahusika na amri ya kuwekwa chini ya uangalizi anaweza kupewa masharti yafuatayo-

(a) kuripoti kwa afisa ustawi wa jamii muhusika katika muda na mahali tajwa;

(b) kuheshimu maelekezo ya afisa ustawi wa jamii;

(c) kutoa taarifa ya mabadiliko yoyote ya anuani, shule au ajira;

(d) kutoondoka katika eneo la makazi bila ruhusa;

(e) kuzuiliwa kuonana au kuwasiliana na mtu au watu waliotajwa;

(f) kuzuiliwa kuingia majengo yaliyotajwa au maeneo yaliyoainishwa; na

(g) kuheshimu masharti ya shule au ya nyumbani.

(3) Mahakama inaweza kutoa amri ya nyongeza inayomtaka mtoto kwenda shule, kuishi pahala fulani, kupata matibabu au ushauri, kuhudhuria program ya kujirekebisha au kujumuika au

kutokutumia kilevi au madawa.

(4) Pale ambapo amri ya kuwa chini ya uangalizi itaonekana na Mahakama kuwa ni hukumu stahiki kwa mtoto, na mzazi, mlezi au ndugu hayuko tayari kumsimamia mtoto, Mahakama itamweka mtoto chini ya usimamizi wa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii wa Wilaya ambayo mtoto anaishi au kama mtoto haishi hapo, wilaya ambayo mtoto anatarajiwa kuishi, au kama hakuna makazi ya kudumu, wilaya ambayo mtoto alikamatwa au wilaya ilipo Mahakama, isipokuwa kwamba endapo mantiki ya Serikali za mitaa imekwisha chukua jukumu la mtoto huyo, itaendelea na jukumu hilo.

(5) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (4), Mahakama inaweza kuchukulia kwamba mamlaka ya Serikali za mitaa imekwisha chukua jukumu la mtoto iwapo afisa ustawi wa jamii amepata mbadala unaofaa katika wilaya kwa ajili ya mtoto na kwamba mamlaka ya Serikali za mitaa imeamua kuchukua jukumu la mtoto huyo.

(6) Mahakama itatoa amri ya kinga ya matoto kwa idara ya ustawi wa jamii husika ambayo itamhifadhi na kumsaidia mtoto.

Ukiukwaji wa amri ya kifungo cha nje

**53.-**(1) Pale ambapo mtoto atakiuka amri ya kifungo cha nje, mtoto huyo anaweza kurudishwa Mahakamani na mwendesha mashtaka.

(2) Baada ya kurudishwa kwa mtoto, Mahakama inaweza-

(a) kuthibitisha amri ya kifungo cha nje;

(b) kubatilisha, kuongeza au kubadilisha sharti lototе la amri; au

(c) kufuta amri na kutoa amri nyingine ya kifungo cha nje kwa kadri Mahakama hiyo itaona inafaa.

(3) Maamuzi yatakapofanyika na Mahakama, taarifa nyingine itaadaliwa na afisa ustawi wa jamii aliyeelekezwa na iwapo afisa ustawi wa jamii hajaelekezwa na mtoto sio mhusika wa amri ya kuwekwa chini ya uangalizi, afisa ustawi wa jamii wa mamlaka ya serikali ya mitaa ambayo mtoto anaishi ataandaa ripoti.

(4) Mahakama itatoa amri ya kifungo kwa mtoto iwapo kuna ukiukwaji wa amri ya kifungo cha nje na iwapo vigezo vya kanuni ya 54 vimethibitika.

Amri ya kupelekwa katika shule ya maadilisho

**54**.-(1) Pale ambapo mtoto ametiwa hatiani-

(a) kwa kosa kubwa kwa kutumia nguvu nyingi au kutokana na hatia hiyo amegundulika kuwa mkosaji wa mara kwa mara, na kosa ambalo amelifanya, kama lingefanywa na mtu mzima, lingeadhibika kwa kifungo; na

(b) Mahakama inaamini kuwa kuna uwezekano mkubwa wa madhara kwa umma,

Mahakama inaweza, kama hatua ya mwisho, na kwa mujibu wa JCR Fomu 14A iliyo ainishwa katika Jedwali la Tatu, kutoa amri kuwa mtoto apelekwe kwenye shule ya maadilisho kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu au hadi hapo mtoto atakapo fikisha miaka kumi na minane, lolote litakalo tangulia kati ya hayo.

(2) Kwa kuzingatia kifungu cha 124 cha Sheria, Mahakama, wakati wa kutoa amri kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), itatoa maelezo yanayohitajika kupitia JCR Fomu 14B iliyo ainishwa katika Jedwali la Tatu.

(3) Hukumu ya kifungo haitatolewa kwa kigezo kuwa mtoto amekosa makazi au malezi.

(4) Pale ambapo mtoto ambaye amehukumiwa kifungo cha nje hana makazi au malezi, Mahakama itaelekeza amri ya kinga ya mtoto kwa idara ya ustawi wa jamii husika kwa mujibu wa Kanuni za 50(7) au 52(6).

(5) Mtoto yeyote aliyewekwa kizuizini kwa kipindi zaidi ya kile kilichoelekezwa katika amri, mtoto huyo atawasilisha maombi katika Mahakama ya wilaya ambayo anaashikiliwa, kwa ajili ya kuachiwa huru mara moja.

(6) Maombi yoyote ya meneja wa shule ya maadilisho ya kuomba mda wa kuwekwa kizuizini uongezwe kwa mwaka mmoja chini ya kifungu cha 127 cha Sheria, yatatolewa katika mazingira ya kipekee na pale ambapo Mahakama imedhirika kuwa ni hatari kwa umma.

(7) Kipindi cha kuwa kizuizini hakitaongezwa kwa vigezo vya ukosefu wa malazi na msaada kwa mtoto.

## SEHEMU YA SABA
### MALEZI

Maombi ya ulezi

**55**.-(1) Mahakama, baada ya kupokea maombi ya malezi chini ya kifungu cha 34 cha Sheria, itatoa amri kuthibitisha malezi ya mtoto na tamko la malezi.

(2) Mahakama itapokea na kuyaamulia maombi ya malezi

chini ya kifungu cha 34 endapo-

(a) mtoto ana makazi ya kudumu Tanzania; au

(b) mtoto amekua mkazi wa Tanzania kwa kipindi cha angalau mwaka mmoja; au

(c) mtu ambaye maombi ya malezi yanamhusu amefariki kabla ya tarehe ya maombi na kabla hajafariki aidha aliishi Tanzania au alikuwa ana makazi ya kudumu Tanzania.

(3) Mahakama, katika kusikiliza maombi ya amri ya malezi, inaweza kwa hiari yake yenyewe kutoa amri ya malezi kwa masharti itakayoona yanafaa.

(4) Mahakama, mbali na ushahidi ulioainishwa katika kifungu cha 35 cha Sheria,inaweza kuzingatia-

(a) tarehe na mahala alipozaliwa mtoto;

(b) majina ya mtoto, yakiwemo majina yote ambayo mtoto alikwishawahi kuwa nayo, na maelezo kuhusiana na mabadiliko ya jina la mtoto;

(c) majina yanayopendekezwa kupewa mtoto wakati wa kufanyika amri ya malezi,kwa kutenganisha jina au majina na jina la ukoo linalopendekezwa;

(d) ridhaa kutoka kwa mjibu maombi ya kufanya maombi ya amri ya malezi;

(e) iwapo mwombaji au mtu ambaye maombi ya malezi yanamhusu anajulikana kwa jina jingine mbali na lile linaloonekana katika cheti chake cha kuzaliwa, jina hilo jingine lazima litajwe katika amri.

(5) Afisa wa Mahakama atatuma nakala ya amri, ikiwemo tamko la malezi kwa Msajili wa Vizazi ndani ya siku ishirini na moja, kuanzia tarehe ambayo hiyo imefanyika.

Utaratibu wa kufanya maombi ya ulezi

**56**.-(1) Maombi ya malezi yatafanyika kwa hati ya maombi iliyoainishwa katika mfumo wa JCR Fomu Na. 6 iliyoko katika Jedwali la Tatu na itajumuisha-

(a) jina na anwani ya mwombaji;

(b) maelezo yanaipa Mahakama mamlaka;

(c) maelezo ya maombi yoyote ya awali yaliyowahi kufanyika;

(d) sababu na madhumuni ya maombi; na

(e) ombi kwa Mahakama.

(2) maombi yatawalishwa katika wilaya ambayo-

(a) mwombaji na mjibu maombi wanaishi; au

(b) mjibu maombi anaishi.

(3) Hakutakuwa na fursa ya kupinga maombi kwa kigezo kuwa mwombaji anataka amri ya tamko tu au kwamba hakukuwa na maombi yatokanayo.

Waombaji wa amri ya malezi

**57.**-(1) Mwombaji katika Sehemu hii ataonesha katika maombi mahusiano yake na mtoto na, kama mwombaji ni mnufaikaji wa maombi, ataeleza sababu za kuomba ridhaa maalum ya kuomba amri ya malezi.

(2) Mahakama, wakati wa kufanya maamuzi ya kumpa mnufaikaji mwenye ridhaa maalum chini ya kifungu cha 34(1) (e) cha Sheria, itasikiliza ushahidi wake na mtu yeyote mwingine kwa kadri Mahakama hiyo itaona inafaa.

(3) Mahakama haitakuwa na jukumu la kufahamisha kuhusu maombi kwa ridhaa maalum kwa mtoto ambaye ni mhusika wa maombi au mtu yeyote mwingine mwenye haki na majukumu ya malezi.

(4) Pale ambapo kuna ridhaa maalum kwa mujibu kifungu cha 34(1)(e) wa Sheria, Mahakama-

(a) itashughulikia maombi hayo ndani ya siku ishirini na nane tangu maombi hayo kuwasilishwa; na

(b) itatoa hukumu kuhusu maombi ndani ya siku tisini baada ya kuwasilisha maombi.

(5) Mahakama, wakati wa kufanya maamuzi ya kutoa ridhaa maalum, itazingatia-

(a) mahusiano ya mwombaji na mtoto;

(b) iwo mapendekezo ya maombi yanaweza kubugudhi maisha ya mtoto kiasi cha kumdhuru; na

(c) uwezekano wowote wa madhara unaoweza kujitokeza kutokana na hati ya maombi kwa mjibu maombi;

(6) Mahakama inapoamua kutoa ridhaa maalum, mnufaika wa maombi atawasilisha maombi ya amri ya malezi kwa mujibu wa Sehemu hii.

(7) Pale ambapo mwombaji ni mtoto wa chini ya umri ya miaka kumi na nane, maombi yatafanyika kwa niaba ya huyo mtoto na rafiki wa jirani wa karibu au mlezi wa kuteuliwa na Mahakama.

(8) Pale ambapo mama wa mtoto mwombaji ni mjibu maombi, mama huyo hato ruhusiwa kuwa rafiki wa jirani wa mtoto.

(9) Ridhaa ya maandishi ya kuwa rafiki wa jirani au mlezi

wa kuteuliwa na Mahakama lazima isainiwe na rafiki wa jirani au mlezi wa kuteuliwa mhusika.

Mamlaka ya kukataa maombi

**58.-**(1) Mahakama, kuhusiana na maombi yoyote ya amri ya malezi au tamko la malezi, itakuwa na mamlaka ya kukataa kusikiliza maombi iwapo itaona kuwa maombi hayo sio kwa manufaa ya mtoto.

(2) Pale ambapo Mahakama itaamua kwamba haitakuwa kwa manufaa ya mtoto kusikiliza maombi ya tamko la malezi, itatoa amri kuwa hakuna maombi yatafanyika na mwombaji mpaka kwa ridhaa maalum ya Mahakama.

Wahusika katika mwenendo

**59.** Pale ambapo maombi ya ulezi yamefanyika na kupewa idhini, wajibu maombi watakuwa-

(a) mtu ambaye ulezi ni juu yake;
(b) mtu yeyote ambaye au anadaiwa kuwa mzazi wa mtu ambaye ulezi ni juu yake isipokuwa pale ambapo mtu huyo ni mleta maombi; na
(c) mlezi yeyote wa mtoto, isipokuwa pale ambapo mleta maombi ni mlezi.

Notisi na wito wa maombi

**60.-**(1) Kila maombi, notisi, wito au nyaraka zilizosainiwa na kuwekewa muhuri wa Mahakama kupitia JCR fomu Na.2 kama ilivyo katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi zitakabidhiwa kwa wajibu maombi ndani ya siku saba za uwasilishwaji kwa mujibu wa utaratibu wa uwasilishaji wa wito chini ya kanuni ya V ya Kanuni.

(2) Pale ambapo mjibu maombi hapatikani, utaratibu ulioainishwa kwenye kanuni ya XVI ya Kanuni utafuatwa.

(3) Mjibu maombi katika maombi yoyote ya tamko la malezi atawasilisha majibu ya maombi ndani ya siku kumi na nne za kupokea maombi na kujumuisha maelezo ya mtu mwingine yeyote ambaye mjibu maombi anaona ni muhimu kuwa mhusika katika maombi au kupewa notisi ya maombi.

(4) Mtu atakayepewa notisi ya mwenendo chini ya kanuni ndogo ya (1), anaweza ndani ya siku kumi na nne tangu ilipotolewa notisi kuomba kuunganishwa kama mhusika.

(5) Pale ambapo mtu ana sababu ya msingi ya kutozingatia muda ulioainishwa kwenye Kanuni hii, au ni vigumu kufanya hivyo, Mahakama kwenye mamlaka yake inaweza kuongeza muda wa kuwasilisha notisi, miito na maombi.

Vipimo vya Vinasaba na vipimo vya kitaabibu

Sheria Na. 8 ya 2009

**61.**-(1) Pale ambapo kuna ubishani juu ya wazazi, na ushahidi uliotolewa Mahakamani wakati wa kusikilizwa hautoshelezi kuamua juu ya wazazi wa mtoto, Mahakama inaweza baada ya kuombwa na mhusika yeyote wa mwenendo wa shauri au Mahakama kwa hiari yake yenyewe kuamuru vipimo vya nasaba au vingine vya kitabibu vifanywe kwa mujibu wa Sheria za Vinasaba vya Binadamu.

(2) Pale ambapo kutatolewa amri ya Mahakama ya kufanya vipimo vya nasaba, sampuli, kama itakavyoamriwa na taasisi husika na vipimo vya nasaba, itatolewa na mama, mtu yeyote anayedai kuwa baba au mama wa mtoto kwa mujibu wa masharti ya Sheria za Vinasaba vya Binadamu.

(3) Mipangilio ya uchukuaji na upimaji wa sampuli utakuwa ni jukumu la mhusika aliyeomba vipimo vifanyike na Mahakama itaainisha ukomo wa muda kwa ajili ya mipangilio ya upimaji.

(4) Mahakama itaamua nani atalipa gharama za upimaji au ni kwa kiasi gani kila upande husika utagharamia.

(5) Pale ambapo mama au mtu mwingine yeyote anayedai au kudaiwa kuwa baba au mama atakataa kutoa sampuli, Mahakama itatoa uamuzi kama itakavyoona sahihi kulingana na mazingira.

Yaliyomo katika taarifa ya vipimo vya Vinasaba

**62.** Taarifa ya vipimo vya vinasaba itajumuisha taarifa zifuatazo-

(a) majina ya wahusika waliopimwa;

(b) tarehe na mazingira ya ukusanyaji sampuli kwa kila mhusika aliyepimwa;

(c) uelekeo wa ubaba au umama kufuatia kufanyika kwa kipimo cha nasaba; na

(d) maelezo ya hitimisho kuhusu ubaba.

## SEHEMU YA NANE
### UANGALIZI NA KUMTEMBELEA MTOTO

Utaratibu wa kufanya maombi ya uangalizi au kutembelea mtoto

**63.**-(1) Maombi ya uangalizi au kutembelea mtoto ya mzazi, mlezi au ndugu ambaye anamtunza mtoto huyo yatafanyika kwa kujaza JCR Fomu Na. 8 kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali laTatu la Kanuni hizi.

(2) Maombi ya uangalizi au kutembelea mtoto yatatiwa saini na muombaji au muwakilishi wake.

(3) Maombi yatasajiliwa Mahakamani katika Wilaya-

(a) ambayo wote muombaji na mtetezi wanamakazi ya kudumu; au

(b) ambayo mtetezi anaishi.

(4) Pale ambapo muombaji ni mtoto wa chini ya umri wa miaka kumi na nane, maombi yatafanyika kwa niaba ya mtoto na rafiki wa karibu au mlezi aliyeteuliwa mahakani.

(5) Pale ambapo baba au mama ni mtetezi kwenye maombi, mama au baba huyo hawezi kusimama kama rafiki wa karibu au mlezi wa mtoto huyo.

(6) Ridhaa ya kimaandishi ya kumsimamia mtoto yatasainiwa na rafiki wa karibu au mlezi aliyeteuliwa na Mahakama.

Mamlaka ya Mahakama kuzingatia maombi ya uangalizi au kutembelea mtoto

**64.** Mahakama inaweza kuyazingatia maombi ya uangalizi au kutembelea mtoto yaliyofanywa chini ya vifungu vya 37 na 38 vya Sheria pale ambapo-

(a) mtoto ana mkazi au kikawaida ana mkazi ndani ya Tanzania; au

(b) mtoto amekuwa ni mkazi wa Tanzania kwa muda usiopungua mwaka mmoja; au

(c) mtoto ameondolewa kimakosa kutoka nchi nyingine au amezuiliwa kimakosa nchiniTanzania.

(2) Mahakama-

(a) itayazingatia maombi yoyote kama hayo ndani ya siku ishirini na nane ya kusajiliwa kwa maombi hayo; na

(b) itatoa hukumu juu ya maombi ndani ya siku arobaini na mbili baada ya kuwasilishwa kwa maombi.

Uwasilishwaji wa maombi

**65.-**(1) Mahakama, ndani ya siku kumi na nne baada ya kuwasilishwa kwa maombi ya uangalizi au kutembelea mtoto, itawasilisha kwa kila mjibu maombi husika na mtu yeyote mwenye maslahi-

(a) nakala ya maombi yenye sahihi na muhuri wa Mahakama ;

(b) tarehe ya kuanza kusikilizwa kwa shauri Mahakamani ambayo haitazidi siku ishirini na nane baada ya maombi kusajiliwa na

(c) taarifa zozote za huduma za usuluhishi zinazopatikana katika eneo hilo, na maelezo ya namna ambavyo huduma hiyo inaweza kupatikana.

(2) Pale ambapo muombaji ni mtoto, mkuu wa Idara wa

Ustawi wa Jamii katika wilaya ambayo mtoto ana makazi ya kudumu atajulishwa juu ya maombi hayo.

(3) Pale ambapo mtoto anaishi na mtu ambaye si muhusika wa shauri la maombi, mtu huyo atachukuliwa kuwa ni mtu mwenye maslahi na atapewa nyaraka zilizotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1).

(4) Pale ambapo mtu mwenye maslahi ametambulika baada ya kuanza kwa shauri, nyaraka zilizotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1) zitakabidhiwa kwa mtu mwenye maslahi ndani ya siku kumi na nne toka siku ya kutambulika.

(5) Endapo mjibu maombi alikua anaishi nje ya Tanzania wakati wa kufanya maombi, muda wa wa uwasilishaji maombi utasogezwa mbele kwa kadri Mahakama itakavyoona inafaa.

(6) Utaratibu wa utoaji na uwasilishaji wa hati ya wito utakuwa kama ilivyoelekezwa chini ya Amri ya Tano ya Kanuni za Mwenendo wa Madai.

(7) Mjibu maombi atasajili majibu ya maombi ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya kuwasilishiwa maombi, na pale ambapo mjibu maombi ataonesha kwamba haikuwa rahisi kujibu ndani ya muda huo, Mahakama inaweza kuongeza muda wa kujibu.

(8) Mjibu maombi katika majibu yake ya maombi anaweza kujumuisha maombi yanayofungamana akiomba amri inayofanana au tofauti.

(9) Mahakama itakuwa na mamlaka ya kutoa juu ya maoni yaliyofungamana na amri yoyote ambayo ingetolewa na muombaji wa maombi.

Maombi ya dharura ya kurejeshwa kwa mtoto

**66**.-(1) Pale ambapo mtoto-

(a) ametolewa au ameshikiliwa na mzazi mmoja bila ridhaa ya mwenzake; au

(b) ametolewa kinyume cha sheria au ameshikiliwa kwa kukiuka amri ya Mahakama,

mzazi anaweza kuiomba Mahakama amri ya dharura ya kwamba mtoto arejeshwe na amri ya uangalizi itolewe.

(2) Maombi yanayofanywa chini ya kanuni hii yanaweza kuwa ya upande mmoja na pale yatakapofanywa wakati Mahakama haijakaa maeneo ambayo mwombaji anaishi, maombi hayo yanaweza kufanywa kwa utaratibu wowote unaofaa kwa Mahakama hiyo na mamlaka yanayofanana**.**

(3) Pale ambapo amri inatengenezwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2)(a), muombaji atasajili maombi wakati ambapo maombi

yanafanywa au wakati ambao Mahakama inaweza kuelekeza.

(4) Nakala yoyote ya amri iliyotengenezwa itatolewa na Mahakama ndani ya masaa arobaini na nane kwa kila mtetezi wa maombi.

(5) Pale ambapo Mahakama itakataa kusikiliza maombi kwa msingi wa upande mmoja, itaelekeza kwamba maombi yasikilizwe pande zote.

Mambo ya kuzingatiwa wakati wa utoaji wa amri wa upande mmoja

**67**.-(1) Mahakama katika kuamua kutoa amri ya upande mmoja itazingatia-

(a) kama maombi yatafanyika kwa notisi lakini kipindi cha muda wa notisi na kujibu utafupishwa;

(b) kama kuna sababu nzuri na ya kujitosheleza kutengeneza amri hiyo;

(c) athari juu ya mtoto; na

(d) kipindi cha muda ambao umeisha tangu kutolewa au kuzuiwa kwa mtoto.

Amri ya muda inayotolewa kwa upande mmoja

**68**.-(1) Pale ambapo maombi yanaombwa ya uangalizi au kutembelea mtoto, na Mahakama imeona kwamba ni kwa maslahi mazuri ya mtoto kutoa amri hiyo, Mahakama inaweza-

(a) kutoa amri ya muda ya uangalizi wa mtoto kwa muombaji chini ya kifungu cha 37 cha Sheria wakati inasubili usikilizaji wa ushauri_unaojumuisha pande zote; na

(b) kutoa amri chini ya mamlaka asili ya sheria kwamba mtoto arudishwe mara moja kwa muombaji.

(2) Pale ambapo amri inatolewa chini ya kanuni ndogo ya 1(a) au (b), amri hiyo-

(a) itaidhinisha afisa wa Mahakama wa ustawi wa jamii kupekua, kuchukua jukumu la kumpeleka mtoto kwa mtu alietajwa kwenye amri; na

(b) itaidhinisha afisa polisi mfawidhi wa wilaya kusaidia afisa wa ustawi wa jamii katika kazi hii.

(3) Pale ambapo amri imetolewa chini ya kanuni ndogo ya (2), nakala ya amri itawasilishwa na Mahakama kwa afisa polisi mfawidhi wa Wilaya na mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii katika wilaya ambayo inaaminika mtoto anapatikana.

(4) Pale ambapo amri ya muda imetolewa upande mmoja na mhusika ambaye hakuwepo anataka kupinga amri hiyo, Mahakama itapanga tarehe ya kusikiliza pande zote ndani ya siku kumi na nne.

Kusikilizwa kwa mara ya kwanza

**69**.-(1) Tarehe ya kusikilizwa kwa mara ya kwanza kwa maombi haitakuwa zaidi ya siku ishirini na nane baada ya maombi kusajiliwa.

(2) Wakati wa kuwafahamisha wahusika tarehe ya kusikilizwa kwa mara ya kwanza, Mahakama-

(a) itatoa taarifa za huduma za usuluhishi zinazopatikana;
(b) itawataarifu wahusika kwamba wanapaswa kujaribu kutatua tofauti zao kwa njia ya usuluhishi kabla ya kusikilizwa kwa mara ya kwanza;
(c) itawataka wahusika na mtu yeyote mwenye maslahi ambaye amepewa wito kusikiliza shauri.

Kuunganishwa kwa mtoto kwenye mwenendo

**70**.-(1) Maombi ya kuunganishwa kwa mtoto katika shauri yanaweza kufanywa na afisa wa ustawi wa jamii kwa niaba ya mamlaka ya Serikali za mitaa, muwakilishi wa mtoto, mlezi anayeteuliwa na Mahakama.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo (1), Mahakama yenyewe inaweza kumfanya mtoto kuwa mhusika katika sheria.

(3) Mahakama itatoa maombi pale ambapo ni kwa maslahi ya mtoto kuunganishwa.

(4) Pale ambapo mtoto ni wa umri unaojitosheleza na ni muelewa, anaweza kuomba kuwa sehemu ya shauri aidha kwa niaba yake mwenyewe au kupitia mwakilishi au mlezi aliyeteuliwa na Mahakama.

(5) Katika kuamua kama mtoto anauelewa wa kutosha, hakimu ataongea na mtoto faragha mbele ya afisa wa ustawi wa jamii.

Kuahirishwa

**71**.-(1) Wakati wa kusikiliza shauri kwa mara ya kwanza Mahakama itawahoji wahusika endapo walikwenda kwa msuluhishi na endapo hawakwenda, pale inapowezekana kufanya hivyo itaahirisha shauri kwa kipindi kisichozidi siku ishirini na nane ili kuwawezesha wahusika kutatua shauri hilo kwa njia ya usuluhishi.

(2) Pale ambapo wahusika wamemuona msuluhishi na ushahidi umetolewa kwamba hawakuweza kutatua tofauti zao, Mahakama itaandelea kusikiza shauri hilo.

Amri ya kutolewa kwa taarifa ya uchunguzi wa kijamii kuhusu uangalizi na kutembelea mtoto

**72**.-(1) Pale ambapo kuna maombi yenye ubishani kuhusu uangalizi au kutembelea mtoto, Mahakama inaweza kuelekeza afisa wa ustawi wa jamii kuandaa taarifa ya uchunguzi wa kijamii.

(2) Afisa wa ustawi wa jamii, wakati anaandaa taarifa atashauriana na-

(a) wahusika wote wa shauri peke yao, na

(b) mtoto peke yake na, kama kuna ulazima na wazazi au wahusika wengine wowote.

(3) Wakati wa kutoa mapendekezo ya uangalizi au kutembelea mtoto maslahi bora ya mtoto yatazingatiwa kwa umuhimu mkubwa.

(4) Mahakama itazingatia taarifa ya uchunguzi wa kijamii kabla ya kufanya maamuzi kuhusiana na uangalizi au kutembelea mtoto.

(5) Afisa wa ustawi wa jamii ambaye ameandaa taarifa ya uchunguzi wa kijamii atakuwa tayari kuwa shahidi Mahakamani, pale ambapo mhusika wa shauri ameomba.

(6) Pale ambapo Mahakama imeamua kukataa mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa ya uchunguzi wa kijamiii itaeleza sababu ya kukataa taarifa ya uchunguzi huo.

Mambo ya kuzingatia wakati wa utolewaji wa amri ya uangalizi na kutembelea mtoto

**73**. Katika kuamua iwapo itoe amri ya uangalizi au kutembelea mtoto, Mahakama inaweza kuzingatia, kama nyongeza ya masuala yaliyoainishwa chini ya kifungu cha 39(1) na 26(2) cha Sheria, yafuatayo-

(a) matarajio na hisia za mtoto;

(b) historia na tabia yoyote ya mtoto ambayo Mahakama itaona ina umuhimu;

(c) mahitaji ya mtoto kimaumbile, kihisia na kielimu;

(d) kuepuka uwezekano wa kubugudhi maisha ya mtoto kwa kubadili uangalizi wa mtoto;

(e) uwezekano wa madhara kwa mtoto unaotokana na mabadiliko ya hali;

(f) kumwezesha kila mzazi na mtu mwingine yeyote ambaye Mahakama inafikiri kwamba suala husika ni kutekeleza mahitaji ya mtoto;

(g) madhara yoyote ambayo mtoto anayapata au anaweza kuyapata;

(h) utayari wa kila mzazi kusaidia na kuwezesha uhusiano

uliopo wa mtoto na wazazi wengine; na

(i) utayari kwa mtu asiye mzazi kumsaidia na kuwezesha uhusiano uliopo wa mtoto na wazazi wengine.

Mamlaka ya Mahakama kutoa amri kwa hiari yake

**74**. Mahakama inaweza-

(a) wakati wa kutoa amri ya uangalizi, amri ya kutembelea mtoto aidha kwa maombi ya mhusika wa shauri au kwa mamlaka yake mwenyewe; na

(b) wakati wa kutoa amri ya kutembelea mtoto amri ya uangalizi wa mtoto aidha kwa maombi ya mhusika au kwa mamlaka yake mwenyewe.

Masharti kwa mtu aliyena amri ya uangalizi

**75**.-(1) Mahakama inaweza, katika kutoa amri ya uangalizi kuhusiana na mtoto, kumruhusu mzazi aliye na uangalizi wa mtoto kufanya maamuzi ya kila siku kuhusiana na mtoto na-

(a) kuamua mahali ambapo mtoto ataishi;

(b) kuamua mahali ambapo mtoto atapewa elimu;

(c) kufanya maamuzi ya kitabibu kuhusiana na mtoto,

Isipokuwa kwamba, Mahakama inaweza kuweka masharti yaliyo na ukomo au ya kawaida katika utekelezaji wa haki hizo.

(2) Mzazi mwenye uangalizi wa mtoto, kabla ya kufanya maamuzi makubwa kuhusiana na maisha ya mtoto, yakijumuisha masuala yaliyomo kwenye kanuni ndogo ya (1), atashauriana na mzazi mwenziye.

(3) Mtu aliye na amri ya uangalizi hatobadili jina la mtoto au-

(a) kusababisha mtotokujulikana kwa jina jipya;

(b) kubadili dini ya mtoto;

(c) kumuondoa mtoto nchini Tanzania kwakipindi kisichozidi siku ishirini na nane;

(d) kukubali mtoto kuolewa; au

(e) kumuweka mtoto chini ya uangalizi wa mwangalizi mwingine bila ya idhini ya mzazi mwenziye au kibali cha Mahakama.

Amri ya kutembelea mtoto

**76**.-(1) Amri ya kutembelea mtoto itaweka wazi siku na muda ambapo mtoto anaweza kutembelewa na mzazi ambaye siyo mwangalizi wake au mtu yeyote mhusika na muda na wakati wa kutembelea mtoto, na amri hiyo itajumuisha taarifa za-

(a) muda wa ziada wa usiku utakaojitokeza wakati wa

kumtembelea mtoto;

(b) kumtembelea mtoto siku za sikukuu;

(c) kumtembelea mtoto wakati wa likizo za shule; au

(d) pale ambapo mtoto hahudhurii shule, muda wowote wa ziada wa kumtembelea mtoto kwa madhumuni ya kuchukua likizo na mtoto.

(2) Bila kujali kanuni ndogo ya (1), amri ya kumtembelea mtoto inaweza kuweka wazi kwamba mtoto anaweza kutembelewa na mzazi asiye mwangalizi wake au mtu yeyote mhusika, katika siku na muda kama watakavyokubaliana kati ya wahusika.

(3) Amri ya kutembelea mtoto inaweza kuweka wazi-

(a) mahali ambapo mtoto atatembelewa;

(b) mpangilio wa kumchukua na kumshusha mtoto kabla na baada ya kutembelewa;

(c) mazuio yote ya-

(i) mahali ambapo mtoto atachukuliwa wakati wa kutembelewa;

(ii) mtu ambaye atamuangalia mtoto wakati wa kutembelewa;

(iii) mtu ambaye atakuwepo wakati mtoto atatembelewa mzazi au mtu yeyote mhusika;

(d) matibabu yoyote au utendaji ambaye lazima apewe mtoto wakati wa kutembelewa; na

(e) masharti mengine ambayo yanaweza kuwa ya muhimu katika maslahi bora ya mtoto.

Mambo ya kuzingatiwa wakati wa kutoa maombi ya kutembelea mtoto

**77.-**(1) Mahakama katika kuamua kutoa maombi ya kutembelea mtoto itazingatia-

(a) maslahi bora ya mtoto;

(b) mahusiano ya mwombaji ya mtoto na familia;

(c) hatari yoyote inayoweza kupendekezwa kwenye maombi itakayovuruga maisha ya mtoto kwa kadri mabayo inaweza kumletea madhara; na

(d) hatari yoyote ya madhara ambayo inaweza kuwa imesababishwa na matokeo ya kufunguliwa kesi kwa mtetezi yeyote kwenye maombi.

(2) Maombi yatafanyika kwa mujibu wa kanuni ya 64 kwa mfumo ulioainishwa kwenye Fomu Na. 11 ya JCR katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

Kuondolewa amri zilizopo

**78**.-(1) Pale ambapo Mahakama itatoa amri ya uangalizi kwa mzazi au mtu muhusika, amri hiyo itakuwa na matokea ya kufuta amri yoyote iliyopo ya malezi au amri ya uangalizi.

(2) Pale ambapo Mahakama itatoa amri ya kumtembelea mtoto, itaelekeza namna ambavyo amri hiyo inafuta amri nyingine zilizopo za kumtembelea mtoto.

Kubadilishwa kwa amri ya uangalizi au amri kutembelea mtoto

**79**.-(1) Pale ambapo amri imetolewa ya uangalizi au kumtembelea mtoto, maombi yanaweza kufanywa, kwa sababu za msingi, na muhusika yeyote katika shauri kubadilisha au kutengua amri hiyo.

(2) Maombi katika kanuni hii yatafanyika kwa mujibu wa kanuni ya 64 kwa mfumo ulioainishwa kwenye Fomu Na. 11 ya JCR katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

Katazo la kufanya maombi mengine bila ya idhini maalum ya Mahakama

**80**.-(1) Mahakama inaweza wakati wa kuondoa maombi ya amri ya uangalizi au kutembelea mtoto, kuamua kwamba hakutakuwa na maombi ya ziada kwa mtu yeyote aliyetajwa kwenye amri kuhusiana na mtoto husika bila idhini maalum ya Mahakama.

(2) Amri chini ya kanuni ndogo (1), itatolewa kama suluhisho la mwisho katika maombi yanayojirudia na yasiyo na sababu ya msingi.

(3) Mahakama wakati wa kufanya maamuzi ya kutoa idhini maalum itazingatia-

(a) maslahi bora ya mtoto;

(b) mahusiano ya mwombaji kwa mtoto na familia;

(c) athari yoyote itakayokuwepo kwenye maombi yaliyopendekezwa yatakayoharibu maisha ya mtoto kwa kadri ambayo inaweza kumletea madhara; na

(d) hatari yoyote ya madhara ambayo inaweza kuwa imesababishwa na matokeo ya kufunguliwa kwa kesi kwa mtetezi yeyote kwenye maombi.

(4) Mahakama itaangalia maombi ya idhini maalum ndani ya siku ishirini na nane toka maombi yasajiliwe na itatoa maamuzi siyo chini ya siku arobaini na mbili baada ya kusajiliwa kwa maombi.

Amri za utekelezaji

**81**.-(1) Maombi yanaweza tolewa Mahakamani ya utekelezaji wa amri chini ya sehemu hii pale ambapo mhusika ameshindwa kutimiza vigezo vya amri vilivyoainishwa kwenye Fomu Na. 9 ya JCR katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

(2) Jukumu la kudhibitisha ukiukwaji wa amri hiyo utafanywa na mwombaji.

(3) Endapo Mahakama imejiridhisha kwamba amri haijatimizwa, Mahakama inaweza kubadili amri hiyo kama itakavyoona inafaa.

Kuondolewa kwa mtoto kutoka katika Jamhuri ya Muungano

**82**. Mtoto ataondolewa nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iwapo tu mzazi au mlezi anayeomba kuondolewa kwa mtoto huyo-

(a) ana ridhaa ya maandishi ya mzazi mwingine au mlezi, isipokuwa kwamba ridhaa hiyo haitazuiliwa bila sababu za msingi; na

(b) amepata idhini ya Mahakamani ya kumuondoa mtoto,

isipokuwa kwamba pale ambapo mtoto ni mhusika wa amri ya uangalizi, mzazi anayemuangalia anaweza kumuondoa mtoto kutoka kwenye Mamlaka ya kisheria kwa muda usiozidi siku ishirini na nane.

(2) Maombi ya ruhusa ya kumuondoa mtoto kutoka Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano yatakayofanywa katika mfumo uliosainishwa kwenye Fomu Na. 17 JCR kwenye Jedwali la Tatu la kanuni hizi.

(3) Katika kuamua kama inaweza kutoa idhini ya kumuondoa mtoto kutoka kwenye mamlaka ya kisheria, Mahakama inaweza kuzingatia-

(a) mambo yaliyomo kwenye kanuni ya 77;

(b) sababu iliyokusudiwa kuondolewa;

(c) matokeo ya kukataliwa kwa mzazi wa mwombaji na mtu yeyote mpya wa familia ya mtoto;

(d) mpangilio uliowekwa wa kuhakikisha uendelevu wa mahusiano na mzazi mwingine.

(4) Amri inayoruhusu kuondolewa kutoka kwenye mamlaka inaweza kuwa-

(a) masharti yanayohusu urefu wakuondolewa; na

(b) mpangilio ulio wa moja kwa moja na usio wa moja kwa moja wa kutembelea mtoto kwa mzazi utataka kuwa ndani ya mamlaka ya kisheria.

(5) Mahakama inaweza kuhitaji kwamba mzazi mwombaji atoe dhamana ili kuhakikisha-

(a) kwamba mtoto atarudishwa mwishoni wakati kuondolewa kumekubalika; na

(b) mpangilio wa kutembelea mtoto uliokubalika katika amri umekamilika.

## SEHEMU YA TISA
### MATUNZO

Maombi ya amri ya matunzo

**83**.-(1) Maombi ya matunzo yanawezwa fanywa chini ya kifungu cha 42 cha Sheria katika mfumo ulisainishwa kwenye Fomu Na. 7 JCR katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

(2) Maombi yanawezwa fanyika dhidi ya mzazi mmoja au wote.

(3) Mahakama itapokea na kuamua maombi ya matunzo ya mtoto chini ya kifungu cha 98(1)(b) cha Sheria pale ambapo wazazi wa mtoto hawajaoana.

(4) Mahakama inaweza kupokea na kuamua maombi ya matunzo ya mtoto pale ambapo wazazi wa mtoto wameoana, na wakati wa maombi pale ambapo hamna maombi ya msingi yaliyofanywa chini ya Sheria ya Ndoa

Mambo ya kuzingatiwa wakati wa utoaji wa amri ya matunzo

**84**.-(1) Mahakama kabla ya kutoa amri ya matunzo itaangalia masuala yote yaliyomo kwenye kifungu cha 44 cha Sheria na mapato au mali za wazazi wote au mtu yeyote ambaye kisheria anawajibu wa kumtunza mtoto.

(2) Mahakama katika kuangalia mali au mapato ya mzazi au mtu yeyote ambaye kisheria ana wajibika kumtunza mtoto itazingatia-

(a) ujira, mshahara, marupurupu, motisha, na posho;
(b) huduma zilizotolewa;
(c) shughuli za biashara;
(d) pensheni na mafao ya kustaafu;
(e) gawio na riba; na
(f) mapato na mali inayohamishika na isiyohamishika kama kodi, kuuzwa kwa mazao ghafi, mazao ya shambani, mifugo, mazao ya maziwa na mazao mengine yanayofanana na mahitaji ya wategemezi wengine.

Taarifa ya uchunguzi wa kijamii ya matunzo

**85**.-(1) Mahakama inaweza kabla ya kutoa amri ya matunzo kwa mujibu wa kifungu cha 45 cha Sheria, kumuomba afisa wa ustawi wa jamii kuandaa taarifa ya uchunguzi ya kijamii kwa madhumuni ya-

(a) kukadiria uwezo wa wazazi wakutoa matunzo na malezi kwa mtoto; na
(b) kuhakikisha usahihi wa taarifa kuhusu mapato na matumizi.

(2) Afisa wa ustawi wa jamii, kabla ya kufanya uchunguzi wowote atatoa notisi ya maandishi kwa nia ya kufanya uchunguzi wa-

(a) mzazi bila uangalizi;
(b) mtu aliyemwangalizi wa mtoto; na
(c) mwajiri wa mzazi mmojawapo.

(3) Afisa wa ustawi wa jamii atawasilisha taarifa yake Mahakamani ndani ya siku kumi na nne kutoka siku ambayo Mahakama ilitoa amri hiyo.

Malipo ya matunzoya mtoto

**86**.-(1) Mahakama ya mtoto itatoa amri ya malipo ya matunzo ya mtoto yafanyike-

(a) kwa mzazi au mtu anayemlea mtoto au mtoto mwenyewe;
(b) kwa au kupatia mkuu wa idara ya ustawi wa jamii; au
(c) kwa, au kupitia mtu mwingine yeyote kama mara kwa mara itakavyoelekeza.

(2) Mahakama itaelekeza kwenye amri muda ambao malipo ya matunzo ya mtoto yatafanywa.

(3) Mahakama itasababisha amri ya matunzo kupitiwa kila mwaka kwa madhumui ya kuhakikisha amri ya matunzo inatekelezwa kubadili makazi, kubadili ajira au biashara au mazingira yoyote muhimu.

Utekelezaji wa matunzo ya mtoto

**87**.-(1) Pale ambapo amri ya matunzo ya kifungu cha 42 cha Sheria na imetolewa na Mahakama na-

(a) mtu aliyeamuliwa kumtunza mtoto ameshindwa kutii amri ya matunzo kwa siku zinazozidi ishirini na nane baada ya amri hiyo kutolewa.
(b) malipo ya matunzo yamepitiliza muda zaidi ya siku ishirini na nane,

maombi yanawezwa fanywa utekelezaji wa amri kwa kutumia Fomu Na. 9 JCR iliyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

(2) Mtu anayefanya maombi kwa mujibu wa kanuni ndogo (1), kabla ya maombi ya utekelezaji wa amri ya matatizo kuombwa, atoe notisi kwa mzazi aliyeshindwa ikimtaka mzazi huyo kutekeleza

amri hiyo.

(3) Wakati wa shauri lolote la matunzo Mahakama imepitisha amri ya ulipaji wa pesa yoyote amri hiyo itatekelezwa kwa namna ileile kama vile imepitishwa kwenye shauri lolote la madai chini ya Sheria ya Madai, na mashauri ya Sheria hiyo inayohusiana na utekelezaji wa amri hizo utatumika sawa na amri ya malipo ya fedha katika shauri lolote la matunzo.

Kubadilish wa na kuondolewa kwa amri ya matunzo

**88**.-(1) Mzazi au mtu aliye na uangalizi wa mtoto au mtu yeyote anayewajibika kisheria na ameteuliwa kumtunza mtoto anaweza kufanya maombi Mahakamani kama mfumo ulioainishwa kwenye Fomu Na. 11 JCR ya Jedwali la Tatu la Kanuni hizi kubadili au kufuta amri ya matunzo kwa misingi ya kubadilika kwa mazingira.

(2) Katika kuamua kama kutoa maombi ya kubadili au kufuta amri ya matunzo chini ya kifungu cha 49 cha Sheria Mahakama itazingatia mambo yafutayo-

(a) mabadiliko yoyote makubwa na msingi tangu kutolewa kwa amri;

(b) mahitaji muhimu ya mtoto; na

(c) uwezo wa kila mzazi kulipa matunzo ya mtoto.

## SEHEMU YA KUMI
### KINGA, MALEZI NA UTARATIBU WA USIMAMIZI WA MTOTO

Uvunjaji wa haki ya mtoto

**89**.-(1) Pale ambapo haki ya mtoto imevunjwa, mkuu wa idara ya ustawi wa jamii kwa niaba ya mamlaka ya serikali ya mtaa au mtu mwenye maslahi anaweza, kwa mujibu wa kifungu cha 95(3) cha Sheria, kufanya maombi Mahakamani ya-

(a) msamaha wowote au kutoa amri kwa kadri mazingira yatakavyoruhusu;

(b) kama ni mzazi, amri ya kwamba mzazi atatekeleza dhamana ya uangalizi na malezi sahihi ya mtoto.

(2) Mamlaka ya serikali ya mtaa inaweza, kwa mujibu wa kifungu cha 95(3) cha Sheria kufanya maombi chini ya kanuni hii pale ambapo-

(a) ustawi wa jamii umemuomba mtu anayevunja haki ya mtoto kuchukua hatua au kutokuchukua hatua na mtu huyo amekataa au ameshindwa kufanya hivyo; na;

(b) suala hilo haliwezi kushughulikiwa chini ya masharti

ya sheria yoyote.

(3) Maombi ya amri chini ya kifungu cha 95(3) cha Sheria yatafanywa katika Fomu Na. 4 JCR ya Jedwali la Tatu la Kanuni hizi na yatajumuisha-

(a) jina na pale panapowezekana, tarehe ya kuzaliwa ya mtoto;
(b) kama inajulikana mahali alipo mtoto;
(c) majina yote yawahusika kwenye maombi pamoja na uhusiano wao kwa mtoto;
(d) maelezo ya kina yakiweka wazi historia ya shauri na haki za mtoto zilizovunjwa; na
(e) msamaha unaoombwa.

(4) Pale ambapo kuna madai yamefanywa kwenye sheria ya kwamba mtoto anateswa au yuko kwenye hatari ya kudhurika, Idara ya Ustawi wa Jamii ya Wilaya ambapo mtoto ana makazi ya kudumu au anapolazimika kuishi itakuwa sehemu ya shauri hilo.

(5) Mahakama inaweza, wakati inatumia mamlaka yake chini ya kifungu cha 95(3)(a) cha Sheria kumpa mtoto ulinzi na kutoa amri yoyote au kuamua suala lolote kuhusu uvunjwaji wa haki za mtoto ikijumuisha, lakini haijazuiliwa kwenye-

(a) amri ya kuzuia kutangazwa;
(b) amri ya kukataza jumuiya isiyoruhusiwa;
(c) amri kuhusiana na matibabu, ikijumuisha vipimo vya vinasaba;
(d) amri ya kuzuia utoroshwaji wa mtoto au usafirishaji haramu wa watoto iwapo shauri husika lina masuala mengine ya msingi yanayohusiana na mambo ya nchi nyingine.
(e) amri ya kurudisha mtoto kwenda na kutoka nchi nyingine;
(f) amri ya kwamba idara ya ustawi wa jamii ifanye uchunguzi wa awali ili kuamua iwapo mtoto amepata au yupo kwenye hatari yakupata madhara makubwa.

(6) Mahakama inaweza wakati inatumia mamlaka yake chini ya kifungu cha 95(3) cha sheria kwamba haki ya kuwa mzazi apewe Kamishna na mzazi anayetumia haki ya kuwa mzazi itazuiliwa kwa kadri ambavyo Mahakama itaona inafaa.

(7) Pale ambapo haki ya kuwa mzazi amepewa Kamishna, Mahakama inaweza kuamuru kwamba kila siku malezi na usimamizi wa mtoto yapewe kwa mtu aliyetajwa au kwa mkuu wa

Idara ya Ustawi wa Jamii, ikizingatia kwamba hakuna hatua yoyote muhimu itakayochukuliwa ya maisha ya mtoto bila idhini ya Mahakama.

(8) Haki ya kuwa mzazi itabaki kwa Kamishna isipokuwa na mpaka Mahakama itoe amri.

(9) Pale ambapo Kamishna au haki ya kuwa mzazi kwa mujibu wa amri iliyotolewa katika kifungu cha 95(3)(4) mtoto hatatolewa kutoka Jamhuri ya Muungano ya Tanzania bila idhini ya Mahakama.

Mtoto anayehitaji ulinzi

**90.** Mtoto atachukuliwa anahitaji uangalizi na ulinzi kama amepata madhara makubwa au yupo kwenye hatari ya kupata madhara makubwa kama ilivyotafsiriwa kwenye kanuni za ulinzi wa mtoto, na moja au zaidi ya mazingira yaliyomo kwenye kifungu cha 16 au 144 cha Sheria yatatumika.

Maombi ya amri ya malezi na uangalizi

**91.-**(1) Maombi ya amri ya malezi au uangalizi yawezwa fanywa na mamlaka za serikali ya mtaa ya wilaya ambapo mtoto ana makazi ya kudumu, au iwapo mtoto hana uangalizi wa wazazi Wilaya ambayo mtoto amepatikana au amepangiwa kama ilivyoainishwa kwenye Fomu Na. 3 JCR ya Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

(2) Watetezi kwenye tukio-

(a) watakuwa wazazi wa mtoto;

(b) atakuwa mlezi yeyote wa mtoto;

(c) atakuwa mtu yeyote anayemlea mtoto mara tu kabla maombi hayajafanywa; na

(d) atakuwa mtoto anayezingatiwa kwenye maombi

(3) Maombi yatajumuisha-

(a) jina na pale panapobidi, tarehe ya kuzaliwa mtoto;

(b) majina yote ya mzazi mtetezi na mhusika yeyote kwenye maombi pamoja na uhusiano wao na mtoto; na

(c) kama maombi ni ya amri ya malezi au uangalizi.

(4) Nyaraka zifuatazo zitasajiliwa na maombi-

(a) maelezo ya awali kutoka kwa afisa wa ustawi na jamii kwa mujibu wa Kanuni za Ulinzi wa Mtoto;

(b) mpango wa malezi au uangalizi wa mtoto, wenye taarifa kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Ulinzi wa Mtoto;

(c) taarifa ya uchunguzi wa awali ulivyofanywa chini ya

Kanuni za ulinzi wa mtoto, iwapo zimemalizika wakati wa maombi;

(d) taarifa ya uchunguzi wa jamii uliofanywa chini ya Kanuni za Ulinzi wa Mtoto, zimekamilika wakati wa maombi;

(e) ushahidi ya kwamba mzazi mlezi au mwangalizi amejulishwa nia ya mamlaka za serikali ya mtaa kufanya maombi kwa amri ya ulezi au angalizi na kwa haki ya kuwakilishwa kwa mujibu wa Kanuni za Ulinzi wa Mtoto,

ukizingatia kwamba pale ambapo maombi yamefanywa kwa msingi wa dharura, nyaraka zitakazohitajika kuambatanishwa kwenye maombi zinaweza kutolewa kwa mujibu wa maelekezo ya Mahakama.

(5) Maombi ya amri ya ulezi au uangalizi yatapewa kwa watetezi na Mahakama ndani ya saa arobaini na nane toka yaliposajiliwa.

Kusikilizwa kwa mara ya kwanza wa maombi

**92.-**(1) Usikilizwaji wa mara ya kwanza utafanyika mapema inavyowezekana baada ya maombi kufanywa na sio zaidi ya saa arobaini na nane baada ya maombi kusajiliwa katika sehemu ambayo Mahakama itapanga muda:

(a) wa nyaraka zinazohitajika katika kanuni ya 91(4) kupelekwa kama nyaraka hizo bado hazijasajiliwa na kupelekewa na muombaji wa mamlaka serikali za mtaa;

(b) ambapo mtetezi yeyote, zaidi ya mtoto ambaye ni mhusika wa shauri atasajili majibu ya maombi, maelezo na ushahidi mwingine wowote ambayo anategemea kutumia; na

(c) ambao muombaji anaweza kusajili maelezo wakati wa kujibu.

(2) Bila kuathiri Kanuni ndogo (1), Mahakama inaweza kuelekeza kwenye masuala yafuatayo:

(a) endapo upelekwaji wa maombi kwa wahusika utasitishwa;

(b) endapo shauri au sehemu yoyote ya shauri itaharakishwa;

(c) endapo mtu mwingine yeyote atakuwa sehemu ya shauri;

(d) uteuzi wa mlezi wa kisheria wa mtoto isipokuwa

kama alishateuliwa mwingine;

(e) kuhudhuria kwa mtoto au mtu mwingine yeyote mbele ya Mahakama;

(f) kusajiliwa kwa ushahidi ukijumuisha ushahidi wowote wa kitaalamu; na

(g) endapo wahusika na wawakilishi wao watakutana wakati wowote wa shauri na madhumuni ya kukutana kwao.

(3) Pale panapowezekana na endapo haitasababisha ucheleweshaji wowote hakimu anayesikiliza shauri kwa mara ya kwanza ataendeleza mwenendo wa kesi mpaka mwisho wa kusikilizwa kwa kesi hiyo.

Maombi ya kujumuishwa kama mjibu hoja

**93.**-(1) Mtu mwenye maslahi anaweza kuiomba Mahakama ruhusa maalum kujumuishwa kama mtetezi kwenye maoni ya amri ya uangalizi na usimamizi wa mtoto.

(2) Mahakama wakati wa kuamua kutoa ruhusa maalum itazingatia-

(a) mahusiano ya muombaji na mtoto;

(b) endapo muombaji ni mwangalizi mzuri wa mtoto;

(c) maoni ya mamlaka ya serikali ya mtaa kuhusu kujumuishwa; na

(d) endapo maslahi muhimu ya mtoto yamepelekwa kwa mtetezi aliyejumuishwa.

Amri ya muda ya malezi au uangalizi

**94.**-(1) Mahakama inaweza, wakati wa kusikilizwa kwa mara ya kwanza kwa maombi ya amri ya malezi au usimamizi au wakati wowote kabla ya usikilizwaji wa mwisho kumalizika, kutoa amri ya malezi wa muda au usimamizi.

(2) Pale ambapo maombi ya amri ya malezi yamefanywa, kufuatia kuondolewa kwa mtoto na kuwekwa sehemu salama na haikuwezekana kumpata mzazi, mlezi au mwangalizi kwa kumpelekea maombi kabla ya kumalizika kwa muda wa amri yakuwekwa kwenye sehemu salama, amri ya dharura ya malezi inaweza fanywa kwa muda wa saa sabini na mbili kuhusu maombi kupelekwa au kusitishwa.

(3) Amri ya malezi ya muda au usimamizi utafanyika kwa muda kama inavyoweza kuainishwa kwenye amri, si zaidi ya muda wa wiki nane kabla siku ya kwanza amri ilivyotolewa.

(4) Amri ya muda inaweza kutolewa upya kwa muda wa

siku ishirini na nane.

(5) Pale ambapo wahusika wamekubaliana kwa maandishi kutolewa upya kwa amri ya muda ya malezi au usimamizi, Mahakama inaweza kutoa amri hiyo bila wahusika kuja mbele ya Mahakama.

(6) Pale ambapo amri ya muda imetolewa na Mahakama, Mahakama inaweza kuelekeza-

(a) Idara ya Ustawi wa Jamii kwa niaba ya mamlaka ya serikali ya mtaa; au

(b) muhusika mwingine yeyote wa shauri,

kuandaa taarifa ya kitabibu au uchunguzi wa kiakili wa mtoto au mtetezi yeyote wa shauri.

Ushahidi wa kitaalam

**95**. Pale ambapo mtoto ni mhusika wa maombi ya amri ya uangalizi au usimamizi mtu hatasababisha mtoto kufanyiwa uchunguzi wa kiafya au kiakili au kufanyiwa tathimini ya madhumuni ya maandalizi kwa ajili ya kutumiwa kwenye sheria bila ruhusa ya Mahakama.

Wahusika kukubaliana kuhusu maelezo ya wahusika kuhusu hoja zinazobishaniwa

**96.** Mahakama itahitaji wahusika kabla ya kumalizika kusikilizwa kwa shauri la maombi, kuandaa nyaraka ambazo zinaonyesha masuala waliyokubaliana na ambayo hawajakubaliana.

Wahusika kusikilizwa

**97**.-(1) Kwa kuzingatia maelekezo yoyote yaliyotelewa chini ya kanuni ndogo ya (2), wahusika na walezi wa mtoto waliochaguliwa kisheria, watatoa ushahidi wao wakati wa kusikilizwa kwa maombi chini ya Sehemu hii kwa amri ifuatayo-

(a) muombaji;

(b) mzazi, mlezi au mwangalizi wa mtoto;

(c) watetezi wengine wa maombi;

(d) mtoto kupitia mlezi aliyeteuliwa kisheria; na

(e) mtoto kama ni sehemu ya shauri na hakuna mlezi aliyeteuliwa kisheria.

(2) Mahakama inaweza kuruhusu shahidi kutoa ushahidi bila kufuata amri iliyotolewa chini ya kanuni ndogo ya (1), pale ambapo ni kwa maslahi bora ya mtoto na ni muhimu kwa maslahi ya haki.

Amri zinazoweza kutolewa kufuatia maombi ya amri ya uangalizi

**98.-**(1) Mahakama inaweza, kwa maombi ya amri ya malezi, kutoa amri-

(a) ya kumuweka mtoto kwa heshima ya mtu ambaye maombi yaliyoombwa kwenye uangalizi wa muombaji, mamlaka ya kiserikali ya mtoto;

(b) ya kumuweka mtoto chini ya usimamizi wa muombaji, mamlaka ya sheria ya mtoto;

(c) ya ukaguzi na uzalishaji kwa mujibu wa sehemu ya kumi na moja ya kanuni hizi; au

(d) ya kutenga kwa mujibu wa Sehemu ya Kumi na Mbili ya Kanuni hizi.

(2) Mahakama inaweza kwa maamuzi yake yenyewe kutoa amri ya usimamizi badala ya malezi, kama itagundua kwamba amri hiyo ni kwa maslahi bora ya mtoto.

(3) Pale ambapo Mahakama imeamua amri ya usimamizi badala ya malezi, itaahirisha shauri hilo kuruhusu serikali ya mtaa kutoa mpango wa usimamizi.

(4) Pale ambapo shauri la amri ya malezi imehairishwa, Mahakama inaweza kutoa amri ya muda ya malezi au amri ya muda ya usimamizi kuhusiana na mtoto husika.

(5) Mahakama haitatoa amri ya malezi kuhusu mtoto mpaka iwe imezingatia mpango wa malezi.

Mtoto kuwa huru kuasiliwa

**99**.-(1) Pale ambapo Mahakama imetoa amri ya malezi na mamlaka ya serikali ya mtaa imesajili ushahidi kwamba watu wote wenye haki na majukumu ya mzazi wamekubaliana mtoto aasiliwe kwa mujibu wa Kanuni za Ulinzi wa Mtoto na kanuni za kuasili mtoto, amri ya malezi itaandika kwamba mtoto yuko huru kuasiliwa na anaweza kuishi na wazazi waliomuasili.

(2) Pale ambapo Mahakama imetoa amri ya malezi wakati mpango wa malezi ni wakuasili, itasitisha kibali cha mzazi cha kuasili na itatoa amri ya kumruhusu mtoto kuasiliwa kama-

(a) mzazi au mlezi hapatikani; au

(b) mmoja au wazazi wote au mlezi hajulikani; au

(c) wazazi au mlezi hana uwezo wa kutoa kibali; na

(d) hamna mtu yeyote mwenye haki na majukumu ya mzazi chini ya makubaliano au amri ya Mahakama inajulikana na inaweza kupatikana.

(3) Mahakama katika kuamua kama mzazi hawezi

kupatikana , itahakikisha kwamba uchunguzi unaofaa umefanyika kwa watu wanaoweza kujua alipo mzazi au mlezi au mtu yeyote mwenye haki na majukumu chini ya makubaliano au amri ya Mahakama anapoishi ikijumuisha wajumbe wa familia na muajiri wake wa mwisho.

(4) Mahakama katika kuamua kama mtu hawezi kutoa kibali itazingatia-

(a) kama mzazi anauwezo wa kutoa kibali; na
(b) kipindi cha muda ambao mzazi hana uwezo wakutafakari mahitaji ya mtoto yaliyoletwa ndani ya kipindi cha kuzaliwa katika familia.

(5) Pale ambapo-

(a) maombi yamefanywa ya amri ya malezi; na
(b) mpango wa malezi ni wa kuasili; na
(c) wazazi, mlezi au mtu mwingine mwenye haki na majukumu chini ya makubaliano au amri ya Mahakama hairuhusu kuasili; na
(d) wazazi mlezi au mtu mwingine mwenye haki na majukumu chini ya makubalino au amri ya Mahakama yakumuacha au kuendelea kumtendea vibaya mtoto au ameshindwa kumlinda mtoto dhidi ya kuachwa au kuendelea kutendewa vibaya na mtu mwingine,

mamlaka ya serikali ya mtaa inaweza kuomba amri ya kumruhusu mtoto kuasiliwa kwa msingi wa kibali kushikiliwa bila sababu.

(6) Mahakama katika kuamua kama mtoto ameachwa au ameendelea kutendwa vibaya itaangalia-

(a) taarifa yoyote ya kijamii, taarifa ya uchunguzi ya kijamii au tathimini ya mtoto na mzazi mlezi au mtu mwingine mwenye haki na majukumu chini ya makubaliano au amri ya Mahakama itachukuliwa na muombaji mamlaka ya serikali ya mtaa au mamlaka ya serikali ya mtaa ambapo mtoto alikaa mwanzo;
(b) kipindi cha muda ambacho mtoto amelelewa nje ya familia yake, kama kipo, na mawasiliano ya kila mara kati ya mtoto na wazazi wakati wote kipindi ambacho mtoto alilelewa nje; na
(c) utumiaji mbaya na vurugu yoyote iliyofanyika dhidi ya mtoto na wazazi wake.

(7) Mahakama katika kuamua kama kibali kilishikiliwa bila sababu kitaangalia-

(a) haki ya mtoto kukua kwenye mazingira ya kifamilia;
(b) mahitaji ya mtoto ya kupata familia ya mbadala ya kudumu;
(c) mahusiano ya mtoto na familia aliyozaliwa; na
(d) uwezekano wa mtoto kuunganishwa na familia aliyozaliwa ndani ya muda unaokidhi mahitaji ya mtoto.

(8) Mahakama, katika kufikia maamuzi yake kama isitishe kibali itachukua ushahidi wa maneno kutoka kwa afisa ustawi wa jamii aliyepatiwa jukumu hilo kwa maslahi bora ya mtoto.

(9) Mahakama, katika kufikia maamuzi kuhusu kusitisha kibali chini ya kanuni, itazingatia kwamba ucheleweshaji wowote wa kutoa maamuzi kuhusu malazi ya mtoto kuhakikisha kama ni kwa maslahi bora ya mtoto.

(10) Mzazi, mlezi au mtu mwingine mwenye haki na majukumu chini ya makubaliano au amri ya Mahakama inaweza, kwa mujibu wa masharti ya Sheria kufanya maombi Mahakamani kutengua amri ya malezi na kutoa amri ya kumruhusu mtoto kuasiliwa.

(11) Pale ambapo kibali kimesitishwa chini ya kanuni hii, na hakuna maombi yoyote yaliyofanywa ya kutengua amri ya malezi au maombi ya kutengua amri hiyo imekataliwa, na rufaa yoyote imekataliwa, Mahakama-
(a) itaweka kumbukumbu kuwa mtoto yuko huru kuasiliwa;
(b) mamlaka ya serikali ya mtaa inaweza kumruhusu mtoto aliyeasiliwa kuishi na wazazi waliomuasili;
(c) kibali cha kuasili kilichotolewa chini ya kanuni hii haitakuwa sehemu ya changamoto katika Mahakama nyingine yoyote.

(12) Pale ambapo mzazi aliyeasili mtoto amefanya maombi ya kuasili au uasili wa wazi, na kibali kilisitishwa chini ya kanuni hii-
(a) hakutakuwa na sharti la kumtaarifu mzazi au mlezi au mtu mwingine mwenye haki au majukumu chini ya makubaliano au amri ya Mahakama kwamba maombi ya kuasili yamesajiliwa na hakuna sharti la kumuweka mzazi, mlezi au mtu mwingine mwenye haki na majukumu chini ya makubaliano au amri ya Mahakama kuwa sehemu ya shauri.

Vigezo vya kutolewa kwa amri ya uangalizi

**100**. Mahakama inaweza kutoa amri ya muda ya uangalizi au usimamizi au amri ya malezi au usimamizi kama imejiridhisha-

(a) kwamba mtoto husika amepata au anaweza kupata madhara makubwa;

(b) kwamba madhara au uwezekano wa kupata madhara hayo umesababishwa na:

(i) malezi au upungufu wa malezi wa mzazi kwa mtoto;

(ii) mtoto yuko nje ya uangalizi wa mzazi; au

(iii) utoaji wa amri hiyo ni kwa maslahi bora ya mtoto.

Haki ya wazazi chini ya amri ya uangalizi

**101**.-(1) Pale ambapo amri ya uangalizi au amri ya uangalizi ya muda inatumika kuhusiana na mtoto, mamlaka ya serikali ya mtaa-

(a) itakuwa na haki na jukumu la mzazi juu ya mtoto; na

(b) itakuwa na mamlaka ya kuamua kiasi ambacho mzazi au mtu yeyote ambaye amepewa haki ya kuwa mzazi na Mahakama atatekeleza haki na wajibu kuhusiana na mtoto.

(2) Mamlaka ya Serikali ya mtaa itazuia tu haki ya kuwa mzazi kwa kiasi ambacho ni muhimu kulinda na kuendeleza ustawi wa mtoto.

(3) Wakati amri ya uangalizi inatumika-

(a) mamlaka ya Serikali ya mtaa au mtu yeyote anayemuangalia mtotohata-

(i) badili majina ya mtoto; au

(ii) badili dini ya mtoto; au

(iii) kubali mtoto huyo kuolewa,

bila amri kutoka Mahakamani;

(b) mamlaka ya serikali ya mtaa hata muondoa mtoto, au kumruhusu mtu yeyote anaefanya jambo kwa niaba ya mamlaka ya serikali ya mtaa kumuondoa mtoto kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, isipokuwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (c) bila idhini ya Mahakama;

(c) kanuni ndogo (b) haitazuia kuondolewa kwa mtoto kwa kuzingatia amri ya malezi kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi kisichozidi siku

ishirini na nne isipokuwa kwamba mtu huyo kapata kibali cha maandishi kutoka mamlaka ya serikali ya mtaa.

(4) Kanuni ndogo (3)(b) haitatumika pale ambapo mpango wa malezi wa mtoto ni kuishi nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(5) Kanuni hii haitatumika pale ambapo mpango wa uangalizi ni kwa ajili ya kuasili na Mahakama imeamuru kwamba idhini ya wazazi wanaokusudia kuasili isitishwe kwa mujibu wa kanuni ya 99.

Kuweka utaratibu wa kumtembelea mtoto aliye chini ya amri ya uangalizi

**102.** Mamlaka ya serikali ya mtaa, kwa maombi ya amri ya uangalizi ya mtoto yaliyoainishwa katika mpango wa uangalizi, mpangilio wa kumtembelea mtoto kati ya mtoto na-

(a) mzazi wake;

(b) mlezi wake;

(c) mtu yeyote ambaye alikuwa anauangalizi wa mtoto mara tu baada ya maombi ya amri ya malezi kufanywa;

(d) mtu mwingine yeyote aliyetajwa ambaye ni muhimu kwa mtoto.

Maombi ya kumtembelea mtoto aliyeko katika uangalizi

**103.-**(1) Mahakama inaweza kwa maombi ya mamlaka ya serikali ya mtaa au mtu yeyote aliyetajwa katika kanuni ya 102(a) mpaka (d) kutoa amri ya kumtembelea mtoto na inaweza kujumuisha muda na sehemu ya kumtembelea.

(2) Mahakama inaweza, kwa maombi ya mamlaka ya serikali ya mtaa au ya mtoto, kutoa amri ikiruhusu mamlaka kukataa kutembelewa mtoto na mtu yeyote aliyetajwa katika kanuni ndogo ya (1) na ametajwa kwa amri.

(3) Mahakama inaweza, wakati inatoa amri ya uangalizi kuhusiana na mtoto, kutoa amri chini ya kanuni hii, hata kama hakuna maombi ya amri hiyo iliyoombwa kuhusiana na mtoto, kama itazingatiwa kwamba amri hiyo inabidi ifanyike.

Muda wa amri ya uangalizi

**104.** Amri ya uangalizi inaweza kufanywa kwa kipindi cha ukomo wa miaka mitatu au mpaka mtoto atakapofikisha umri wa miaka kumi na nane yoyote itakayoanza.

Uombaji wa ziada wa amri ya

**105.-**(1) Mamlaka ya serikali ya mtaa inaweza kufanya maombi ya amri ya uangalizi mara baada ya kuisha kwa amri ya kwanza au amri iliyopo ya uangalizi kuisha isipokuwa kwamba

uangalizi

mtoto yupo chini ya miaka kumi na nane wakati wa maombi hayo.

(2) Maombi yatasajiliwa na mamlaka ya serikali ya mtaa ambayo ilikuwa na amri halisi, isipokuwa kwamba pale ambapo kipindi cha muda kati ya kwisha kwa amri halisi na maombi ya amri mpya, maombi yatafanywa na mamlaka ya serikali ya mtaa pale ambapo mtoto ana makazi ya kawaida, alipatikana au alipangiwa.

(3) Maombi yatafanywa kwa mujibu wa kanuni ya 91 na yatajumuisha-

(a) maelezo yanayoeleza sababu kwa nini maombi yamefanywa kwa mara ya pili au kwa amri ya malezi iliyopo;

(b) uchunguzi wa uteuzi wa kijamii na kifamilia uliofanywa kwa madhumuni ya kutenganisha;

(c) mpango wa malezi utakaopanga ambao utafanywa kwa mtoto ukiwa na taarifa zilizoainishwa kwenye Kanuni ya Ulinzi wa Mtoto;

(d) muhtasari wa maandalizi ya kuondolewa kwa kesi ikapitia kwenye mkutano uliofanywa kwa mujibu wa Kanuni ya Ulinzi wa Mtoto chini ya amri ya malezi iliyopita; na

(e) nakala ya amri halisi na amri ya maombi yoyote ya ziada yaliyofanywa na Mahakama.

Kuondolewa kwa amri ya uangalizi

**106.-**(1) Maombi ya kuondolewa kwa amri ya uangalizi chini ya kifungu cha 23 cha Sheria yatafanyika katika mfumo ulioainishwa kwenye Fomu Na. 11 JCR katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi na maelezo yanayoelezea sababu ya kuondolewa na mpangilio utakaofanywa kwa mtoto utajumuishwa.

(2) Pale maombi ya kuondolewa amri ya uangalizi yamefanywa na mtoto-

(a) mamlaka ya serikali ya mtaa itafanywa sehemu ya shauri hilo; na

(b) mtoto atasaidiwa katika mwenendo na mlezi aliyeteuliwa na Mahakama.

(3) Pale ambapo mtoto ameomba amri ya malezi kuondolewa na hana uangalizi aliyeteuliwa na Mahakama, Mahakama itamteua mlezi ikipokea maombi na pale itakapowezekana itamteua mlezi yule yule ambaye alimwakilisha mtoto kwenye shauri la uangalizi.

(4) Pale ambapo maombi ya kuondolewa kwa amri ya

malezi ya mtoto yamefanywa na mzazi, mtoto na mamlaka ya serikali ya mtaa watatajwa kama wahusika wa shauri hilo.

(5) Pale ambapo mamlaka ya serikali ya mtaa imeomba amri ya malezi iondolewe-

(a) mtoto na wazazi au mlezi watafanywa wahusika wa sehemu ya shauri, na mlezi wa mtoto aliyeteuliwa na Mahakama kwa ajili ya mtoto;

(b) itasajili mpango wa malezi kuondolewa kwa mujibu wa Kanuni ya Ulinzi wa Mtoto.

(6) Amri ya maelezi itaondolewa pale tu-

(a) Mahakama imethibitisha kwamba amri ya malezi haihitajiki tena kwa ulinzi na usalama wa mtoto;

(b) mpango wa malezi, ulinzi utakapoondolewa na kuendeleza usalama wa mtoto; na

(c) kondolewa huko ni kwa maslahi bora ya mtoto.

Amri ya usimamizi

**107.-**(1) Amri ya usimamizi inaweza fanywa kuzuia madhara yatakayotokea kwa mtoto wakati mtoto amebaki nyumbani kwenye uangalizi wa mzazi; mlezi au ndugu.

(2) Amri ya usimamizi haitahitaji mtoto aishi sehemu nyingine yoyote zaidi ya kuishi na familia yake.

Amri zinazoweza kutolewa baada ya kuwasilishwa kwa maombi ya amri ya usimamizi

**108.** Mahakama inaweza wakati wa maombi ya amri ya usimamizi, kutoa amri-

(a) ya kumuweka mtoto chini ya usimamizi wa mwombaji mamlaka ya serikali ya mtaa;

(b) ya kumuweka mtoto kwa heshima ya mtu atakayefanya maombi ya malezi kwa mamlaka ya serikali ya mtaa;

(c) ya upekuzi na kutoa kwa mujibu wa kanuni ya 111; au

(d) ya kuzuia kwa mujibu wa kanuni ya 116.

(2) Mahakama inaweza kutoa amriya badala ya amri ya usimamizi kwa mamlaka iliyonayo kama amri hiyo ni kwa maslahi bora ya mtoto.

(3) Mahakama kabla ya kutoa amri ya malezi kwa mamlaka iliyonayo, itaahirisha shauri kuruhusu mamlaka ya serikali ya mtaa kuleta mpango wa malezi.

(4) Pale ambapo shauri la amri ya usimamizi limeahirishwa,

Mahakama inaweza kutoa amri ya muda ya usimamizi au amri ya muda wa malezi kuhusiana na mtoto husika.

(5) Mahakama haitatoa amri ya usimamizi mpaka itakapozingatia mpango wa usimamizi.

Muda wa amri ya usimamizi

**109**.-(1) Amri ya usimamizi inaweza tolewa katika kipindi cha mwaka mmoja au mpaka mtoto afikishe umri wa miaka kumi na nane kwa kuzingatia kitakachoanza.

(2) Amri inayorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) itafanywa kwa kibali cha mzazi au mlezi.

(3) Amri ya usimamizi inawezwa kusogezwa kwa maombi yatakayofanywa na mamlaka ya serikali ya mtaa kwa muda wa zaidi wa kipindi cha mwaka mmoja au mpaka pale mtoto atakapofikisha umri wa miaka kumi na nane, lolote kwa kuzingatia kitakachoanza.

(4) Mahakama itaongeza muda wa amri pale tu mambo yaliyomo kwenye kanuni ya 100 yanaendelea kutumika na-

(a) kuongeza huko kwa muda ni kwa maslahi bora ya mtoto;

(b) mzazi au mlezi amekubali; na

(c) mtoto amekubali.

Mamlaka ya usimamizi

**110**.-(1) Amri ya usimamizi itamueka mtoto chini ya usimamizi wa mmalaka ya serikali ya mtaa ambayo imefanya maombi,

isipokuwa kwamba pale ambapo mtoto ataishi sehemu tofauti ya mamlaka ya serikali ya mtaa kwa wakati wa amri, mtoto atawekwa chini ya usimamizi wa mamlaka ya serikali hiyo.

(2) Pale ambapo mpango wa usimamizi ni kwa mtoto kuishi katika mamlaka ya serikali ya mtaa nyingine, serikali hiyo ya mtaa itajulishwa na muombaji mamlaka ya serikali ya mtaa wakati mpango wa usimamizi unasajiliwa Mahakamani.

(3) Mamlaka ya serikali ya mtaa nyingine itakuwa na haki ya kuomba ifanywe sehemu ya shauri hilo.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
### AMRI YA UPEKUZI NA KUTOA

Maombi ya amri ya upekuzi na kutoa

**111**.-(1) Pale ambapo mamlaka ya serikali za mitaa imefanya maombi ya amri ya malezi au amri ya usimamizi, mamlaka ya serikali za mitaa inaweza kuomba amri ya kutoa chini ya kifungu cha 29(2) cha Sheria kwa mfumo ulioainishwa katika JCR Fomu Na.

5 kwenye Jedwali la Tatu la kanuni endapo-

(a) kuna sababu za msingi za kuamini kwamba mtoto anaathirika au yupo kwenye hatari ya kupata madhara makubwa;

(b) mamlaka ya serikali ya mtaa imeamua kufanya uchunguzi; na

(c) mamlaka ya serikali ya mtaa imeamua kufanya mamlaka yake chini ya kifungu cha 96(1) cha Sheria kupekua nyumba ambapo mtoto amewekwa na ameshindwa kupatikana.

(2) Maombi-

(a) yatataja jina la mtoto;

(b) yatataja kila mzazi au mlezi na mtu yeyote anayeaminika kumlea mtoto na ataweka anuani yake na maelezo ya mawasiliano mengine yoyote;

(c) yatakuwa na masuala ambayo mamlaka ya serikali ya mtaa itatuma kuidhinisha mtoto anaumwa au anaweza kupata madhara makubwa na madhara anayoweza kupata kama upekuzi au amri ya kutoa mtoto haitatolewa;

(d) yatataja majina ya nyumba ambapo inaaminika mtoto amewekwa; na

(e) juhudi zilizofanywa kumtafuta mtoto.

Mamlaka ya Mahakama baada ya kutolewa kwa ombi la amri ya upekuzi na kumtoa mtoto

**112**. Pale ambapo Mahakama imejiridhisha kwamba masharti yaliyomo kwenye kanuni ya 111 (1) yamefuatwa, inaweza-

(a) kuipa mamlaka ya serikali ya mtaa mamlaka ya kuingia kwenye nyumba yoyote na kumuondoa mtoto, au mtoto mwingine yeyote aliyekutwa humo ambaye anaumwa au yupo katika athari ya kupata madhara makubwa, kwenda sehemu salama; au

(b) kumtaka mzazi au mlezi kumleta mtoto katika sehemu na muda utakaoamuliwa na Mahakama na sio zaidi ya siku saba baada ya amri kutolewa.

Amri ya upekuzi na ya kutoa inayotolewa kwa upande mmoja

**113.-**(1) Pale ambapo mamlaka ya serikali ya mitaa inasababu ya msingi kuamini kuwa iwapo mzazi, mlezi au muangalizi amejulishwa kuhusu maombi ya amri ya upekuzi na kutoa mtu huyo atamuondoa mtoto kutoka katika nyumba hiyo aliyopo wakati huo, mamlaka ya serikali ya mtaa inaweza kuomba

maombi ya upande mmoja Mahakamani au, kama Mahakama haijakaa kwenye Mahakama iliyo na mamlaka.

(2) Maombi ya upande mmoja yatasikilizwa na Mahakama siku hiyo yatakaposajiliwa.

(3) Kama amri ya upande mmoja imefanywa na Mahakama, amri hiyo inaweza kutekelezwa, lakini mzazi, mlezi au muuangalizi ataoneshwa amri wakati afisa wa ustawi wa jamii ameingia kwenye nyumba.

(4) Pale ambapo amri ya upande mmoja imetolewa, mzazi mlezi au muangalizi atakuwa na haki ya maombi ya kutenguliwa kwa amri ya upekuzi na kumtoa mtoto Mahakamani ndani ya saa sabini na mbili toka amri ya kukazwa hukumu ilipotolewa.

Utaratibu wa kutolewa kwa amri ya upekuzi na kutoa kwa pande zote

**114**.-(1) Maombi yaliyofanywa pande zote yatasikilizwa ndani ya saa arobaini na nane baada ya notisi kutolewa.

(2) Pale ambapo hatua zote muhimu zimechukuliwa za kumpata mzazi, mlezi au muangalizi kwa madhumuni ya kupeleka notisi zimeshindikana na Mahakama imejulishwa kuhusu hilo, maombi yatasikilizwa na Mahakama siku iliyojulishwa.

Kusimamishwa kwa maombi ya amri ya malezi na uangalizi

**115**.-(1) Pale ambapo amri ya upekuzi na kutoa imefanyika, maombi ya amri ya malezi au uangalizi yanaweza kusimamishwa au kuondolewa na Mahakama.

(2) Pale ambapo Mahakama imeamua kusimamisha maombi ya amri ya malezi na uangalizi, Mahakama-

(a) itapanga muda wa kusimamishwa kwa maombi hayo;

(b) itatoa sababu za kusimamishwa.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
### AMRI YA UTENGAJI

Maombi ya amri yautengaji

**116**.-(1) Pale ambapo maombi ya amri ya uangalizi au amri ya usimamizi au amri ya muda ya uangalizi au usimamizi imefanyika na upo ushahidi kuwa mtoto anadhurika au yupo katika hatari ya kupata madhara makubwa, na kwamba madhara hayo makubwa yanaweza kuondoshwa kama mtu anayetajwa akiondolewa katika makazi ya mtoto au amezuiliwa kuwa na mawasiliano na mtoto, maombi ya amri ya kutenga chini ya kifungu cha 28 cha cha Sheria yanaweza kufanywa na-

(a) mamlaka ya serikali za mitaa;

(b) mzazi mlezi au mwangalizi; au

(c) mtoto ambaye ni muhusika wa shauri la maombi ya amri ya malezi na uangalizi.

(2) Mtetezi wa maombi atakuwa mtu ambaye mwombaji anataka atengwe na inaweza kujumuisha mtu ambaye sio muhusika na shauri la malezi na uangalizi.

(3) Maombi ya amri ya malezi au uangalizi yatafanyika kwa kujaza JCR Fomu Na 10 Na. 10 kama ilivyo inavyoenekana katika Jedwali la Tatu pamoja na ushahidi wa kiapo kithibitishe maombi.

(4) Maombi yatawasilishwa na Mahakama kwa utetezi ndani ya saa sabini na mbili, isipokuwa kama maombi niya upande mmoja na suala litasikilizwa ndaniya saa sabini na mbili tangu maombi hayo kupokelewa.

Maombi ya amri ya kuzuia inayotolewa kwa fadhila ya upendeleo

**117**.-(1) Pale ambapo kuna umuhimu wa kumlinda mtoto au mwangalizi wa mtoto, maombi ya amri ya kutenga yanaweza fanyika kwa upande mmoja.

(2) Pale ambapo amri ya kutenga imetolewa kwa upande mmoja Mahakama itatoa amri hiyo kwa mtu muhusika na kumfahamisha mtu huyo haki yake ya kuomba kugeuza au kufuta.

(3) Pale ambapo Mahakama itakataa kutoa amri ya upande mmoja, itaelekeza kwamba usikilizwaji pande mbili ufanyike kuhusiana na maombi hayo katika tarehe itakayopangwa.

Vigezo vya utoaji wa amri ya kutenga

**118**. Pale ambapo katika maombi ya maelezo au uangalizi, Mahakama inaweza itakaporidhika-

(a) kwamba ustawi watoto unaweza kulindwa kwa kumuondoa mtu aliyetajwa kutoka katika makazi ya mtoto au kuzuia mtu kuingia kwenye makazi;

